# Uelekeo

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*



## Waziri Mkuu 'aachia ngazi'

Uk. 19

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00055 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Machi 13 - 19, 2024 |

## Majiji matano kufungwa kamera



Uk. 2

## DC aingilia kati mgomo daladala



Uk. 2

## Rungu lawashukia mgambo waliodaiwa kunyanyasa raia Geita



Uk. 3



# Ziara za Makonda mikoani zawaamsha watendaji

Zilitengwa zaidi ya Sh. bilioni 42.5 na zote zimeshalipwa hivi tunavyozungumza hadi takwimu za leo...

Uk. 4

# Samia kamili kumtua mama ndoo kichwani

■ Amwaga bil. 2.238/- miradi mitano ya maji Songea

Uk. 4



# DC aingilia kati mgomo daladala

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

MKUU wa Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza, Amina Makilagi, ameingilia kati mgomo wa mabasi maarufu kama 'daladala' akiwataka madereva wa usafiri huo, kuacha na kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria.

Akizungumza na vyombo vya habari jijini hapa jana, Amina alisema wamekubaliana na uongozi wa madereva wa daladala wamalize mgomo huo.

''Tumekubaliana kwa pamoja magari yote yarudi barabarani ndani ya saa mbili tokea hivi sasa. Saa nane kamili madereva wote wanatakiwa kurejea barabarani," alisema.

Alisema dereva yeyote atakayekaidi agizo la serikali,atawajibishwa.

"Tumewaelekeza polisi katika maeneo mbalimbali, wasimamie suala la usalama," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Wamiliki wa Wasafirishaji Mkoa wa Mwanza, Yusuph Lupiliya, alisema walipokea taarifa ya vipeperushi kuwa Machi 11, mwaka huu kutakuwa na mgomo wa daladala ila hajui taarifa hiyo ilitolewa na nani.

"Tulipata taarifa za mgomo tangu juzi, lakini hatujui ni nani aliyeandika vipeperushi hivi na kusambaza. Madereva wetu wameweka mgomo huu bila taarifa, sisi tuliwaambia wasigome, kiukweli wenzetu wamekiuka," alisema.

Aliahidi watazungumza na madereva wa daladala ili warejee kazini ifikapo saa 8:00 alasiri (jana)



Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza, Amina Makilagi.

> **Tulipata taarifa za mgomo tangu juzi, lakini hatujui ni nani aliyeandika vipeperushi hivi na kusambaza. Madereva wetu wameweka mgomo huu bila taarifa, sisi tuliwaambia wasigome, kiukweli wenzetu wamekiuka.**



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni.

# Majiji matano kufungwa kamera kudhibiti uhalifu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imepanga kufunga kamera maalum mikoa yote nchini na kwa kuanzia zitafungwa katika majiji matano ili kudhibiti matukio ya uhalifu, ujambazi, wizi na ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliyasema hayo baada ua kukutana na Kikosi Kazi cha Miji Salama kinachoratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa ufungaji wa kamera za kuzuia uhalifu.

Alisema kamera hizo za awali, zitafungwa katika majiji matano ili kudhibiti matukio ya uhalifu ukiwemo ujambazi, ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani, wizi na matukio mengine ya kiuhalifu.

Aliyataja baadhi ya majiji hayo kuwa ni Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza na Arusha huku lengo likiwa ni kufunga kamera hizo katika mikoa yote nchini kwa siku zijazo.

Alisema kuna maeneo ambayo yanatakiwa yawe na udhibiti wa uhalifu hasa kwa kutumia teknolojia na baadhi ya nchi tayari wana mfumo huo na wameanza kufanikiwa kudhibiti uhalifu na makosa ya ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani.

"Serikali tumeanza jitihada za kufunga kamera, sasa mkiwa wajumbe wa kikosi kazi, mfahamu mna jukumu kubwa kwa nchi kuhakikisha mradi huu unatekelezeka ili uwe na manufaa kwa nchi yetu," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini Camilius Wambura, aliagiza wajumbe wa kikosi kazi hicho kuhakikisha wanaupitia vizuri mkataba wa ufungaji wa kamera hizo.

# Balozi Japan nchini 'aiuma sikio' Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Japan nchini, Yasushi Misawa, ametoa ushauri kwa Tanzania ili iweze kupata maendeleo zaidi inatakiwa kuboresha maeneo ya kimkakati ikiwemo viwanda, afya, mazingira, elimu na sekta muhimu kwa ujumla.

Akizungumza wakati wa Mkutano wa mwaka wa Shirikisho la Watanzania wanufaika wa programu za mafunzo ya JICA (JATA,) Balozi Misawa, alisema hatua ya maendeleo ambayo nchi nyingi za Bara la Asia zimepitia ikiwemo Japan, zimetokana na uboreshaji wa miundombinu, sera za maendeleo ya viwanda, sekta ya rasilimali watu pamoja na mafunzo ya ufundi.

Aidha, alisema kupitia Shirika la Maendeleo la Japan Tanzania (JICA) wataendelea kutoa mafunzo ya ujuzi kwa Watanzania na kuwezesha miradi ya kijamii na kiuchumi.

Alisema wataendelea kufanikisha miradi kupitia wanafunzi waliowapa ufadhili ikiwemo mradi wa Hatua Project.

"JICA imechangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii ikijikita katika rasilimali watu na kumekuwa na fursa nyingi za mafunzo na miradi na siku ya leo (jana), nina furaha kushiriki na kujua kutoka kwa wanachama wa JATA ambapo kuna miradi kama Hatua ulioanzishwa kutatua matatizo ya wananchi na hii inaendana na mikakati yetu," alisema.

Alisema tayari wadau kutoka Japan na serikali, walijadili kuhusu changamoto za kiuchumi na kijamii ambapo watafanikiwa kutokana na ujuzi waliotoa na uzoefu walionao.

Katika hatua nyingine, Balozi Misawa alisema uhusiano bora baina ya Tanzania na Japan, umekuwa ukichangia maendeleo ya kijamii na uchumi kupitia miradi mbalimbali.

Alitaja miradi ya Hatua inayotekelezwa na wanachama wa JATA kuwa ina manufaa kwa Watanzania kwa vile inalenga kutatua changamoto za kijamii ambayo ni moja ya mkakati wa JICA.

Akizungumza katika mkutano huo, Mwenyekiti wa JATA, Gregory Mlay, alisema shirikisho hilo limewakusanya Watanzania waliopata fursa ya kusoma Japan.

Alisema mradi wa Hatua ulianza mwaka 2022 kwa miradi mitano ambayo miradi miwili ilitekelezwa mwaka 2022 na mitatu ilitekelezwa mwaka 2023 kwa lengo na kupata fursa ya kutumia teknolojia waliyoipata Japan kwa manufaa ya Tanzania.

Tangu kuanzishwa kwa JICA 1962 hadi mwaka 2022, jumla ya wanafunzi wa Kitanzania 147,863 wamepewa ufadhili wa masomo na shirika hilo katika nchi mbalimbali duniani.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Utumishi, Leila Maviki, alisema serikali inathamini jitihada za serikali ya Japan katika kuchochea maendeleo ya Tanzania kupitia fursa za masomo na mafunzo yatolewayo kwa Watanzania ikiwemo watumishi wa umma ambao wamepata mafunzo kupitia JICA katika uga za afya, Tehama, sekta ya maji na kilimo.



Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa.

# Rungu lawashukia mgambo waliodaiwa kunyanyasa raia

**Na Mwandishi Wetu, Geita**

MALALAMIKO dhidi ya baadhi ya mgambo mkoani Geita wakidaiwa kunyanyasa wajasiriamali kwa kuwashambulia na kuomba `mlungula', yamefikishwa kwa Mkuu wa Mkoa huo, Martine Shigela.

Shigela aliyekwenda kusikiliza kero za wananchi katika Jimbo la Geita alipokeolinda soko la wajasiriamali na ukusanyaji wa fedha za ujenzi wa maendeleo katika Kata ya Nyawilimirwa wilayani Geita katika mkutano wake wa hadhara uliofanyika juzi ambao ulikuwa mahususi kusikiliza kero za wananchi.

Alielezwa kuwa mgambo hao watatu wanatuhumiwa kwa makosa ya kuwashambulia wananchi wawili kwa madai ya kushindwa kutoa mchango.

Katika mkutano huo, Pendo Michael na Mohamed Rashid, wakiwa waathirika wa matukio ya unyanyasaji wa mgambo hao, walimweleza Mkuu wa Mkoa Shigela mbele ya wananchi juu ya kuwepo kwa mgambo ambao wameshindwa kufanya kazi yao kwa uadilifu.

"Kuna watu wale migambo walifika kwangu kudai pesa ya mchango kwamba wanadai pesa ya mchango Sh. 7,000, nikawaambia mume wangu hayupo, wakasema haya tupe namba zake za simu, nikawapa, wakaongea naye, walipomaliza kuongea naye, wakaishika baiskeli yangu waipeleke, nikawaambia baiskeli nimekodi siyo yangu, naomba mnivumile niende sokoni nikawatafute wateja wa kununua mahindi niwaletee hiyo pesa, lakini walikataa," alidai.

"Ndugu Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, nilipigwa sana, nilidhalilishwa sana," alisema.

Mkuu wa Kituo cha Polisi Nyawilimirwa Inspekta Solomon Lulemkamu, athibitisha kuwepo kwa tuhuma hizo huku akikiri kuwakamata na kuwafikisha mahakamani mgambo hao.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana na raia wema katika kubaini na kuwakamata wahalifu wote katika kata hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Geita Martine Shigela, ameiagiza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kukaa na kuleta taarifa za askari hao ikiwemo majina pamoja na namba zao na kuondolewa kazini na kubaki kuwa raia wa kawaida ili kufuatilia mienendo yao pamoja na tabia zao.

"Kikao kijacho cha Kamati ya Usalama cha Mkoa, DC unayekaimu hapa nataka mniletee majina ya mgambo hao na namba zao za simu ili wavuliwe nyadhifa zao na kubaki kuwa raia wa kawaida na watafuatiliwa mienendo yao," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Geita Martine Shigela.

# Mbaroni kwa tuhuma za wizi, utoroshaji mifugo

**Na Abel Paul, Jeshi la Polisi, Shinyanga.**

WATU kadhaa wametiwa mbaroni kwa tuhuma za wizi na utoroshaji wa Mifugo nje ya nchi.

Jeshi la Polisi Kikosi cha Kuzuia Wizi wa Mifugo (STPU), limesema litaendelea kushirikiana na wananchi kwa karibu ili kudhibiti uhalifu huo hapa nchini.

Akitoa taarifa hiyo jana, Kamanda wa Polisi kikosi hicho, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi SACP, Simon Pasua, aLIsema Jeshi hilo linawashikilia watuhumiwa hao wa wizi wa mifugo katika maeneo tofauti nchini

SACP Pasua alitoa taarifa hiyo baada ya kutembelea mnada wa Tinde uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Hata hivyo, Kamanda Pasua hakutaja majina ya watuhumiwa hao kwa sababu za kiuchunguzi na kuahidi kuwa kikosi hicho kitaendelea kuwakamata wote watakaobainika kujihusisha na wizi wa mifugo.

Aidha, aliwaomba wananchi kote nchini kuendelea kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi juu ya baadhi ya watu wanaojihusisha na wizi wa mifugo na kuitorosha nje ya nchi.

Kwa upande wake, Ofisa Biashara kutoka Shinyanga Vijijini, Upendo Milisho, alisema wananchi na wafanyabiashara mifugo katika mnada wa Tinde, wamekuwa na mwitikio chanya katika ulipaji ushuru kwa kielektroniki mnadani hapo.

Naye Afisa Mapato Wilaya ya Shinyanga, Victor Mollel, mbali ya kukishukuru Kikosi cha Kuzuia Wizi wa Mifugo, alisema Jeshi la Polisi pamoja na wananchi, wameendelea kudhibiti uhalifu katika eneo hilo la mnada wa Tinde, kitendo kilichoufanya mnada huo kuwa miongoni mwa minada yenye kukusanya mapato vizuri na usalama wa kutosha.



# Ziara za Makonda mikoani zawaamsha watendaji

**Na Mwandishi Wetu**

AWAMU ya kwanza ya ziara za Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda, alizofanya katika baadhi ya mikoa, zimetajwa kuongeza utendaji kwa watumishi wa serikali wakiwemo mawaziri.

Katika ziara zake kwa nyakati tofauti kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi, Makonda alitoa maagizo kwa mawaziri, wakuu wa mikoa na wakurugenzi kuzipatia ufumbuzi.

Moja ya kero alizosikiliza akiwa mkoani Dodoma, ni migororo ya ardhi, hatua ambayo ilimlazimu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, kuanza utekelezaji wa maagizo ya CCM.

Waziri Silaa alipewa miezi miwili awe amemaliza migogoro hiyo ya ardhi na katika kutekeleza agizo hilo, alisema ofisi yake imeanzisha kliniki ya ardhi ambayo itawawezesha wananchi kupata huduma mahali pamoja.

Aidha, Waziri Silaa alimwelezekeza Katibu Mkuu kutoka maofisini na kwenda kwa wananchi kusikiliza kero zao.

Akiwa mkoani Kagera, Makonda alizikiliza kero za wananchi kuhusu ukosefu wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ambapo alimipigia simu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni kutoa ufafanuzi wa suala hilo.

Akijibu malalamiko hayo, Waziri Masauni alisema tatizo limemalizwa na Serikali.

Alidokeza kuwa shida kubwa ilikuwa ni mkandarasi anayezalisha kadi alikuwa hajalipwa, lakini sasa ameshalipwa.

"Zilitengwa zaidi ya Sh. bilioni 42.5 na zote zimeshalipwa hivi tunavyozungumza hadi takwimu za leo (wakati huo), kadi zilizoingia nchini milioni tano na jumla ya Watanzania milioni 16 ambao wana kadi. Ikifika Desemba mwaka huu (mwaka jana), watu wote watapatiwa kadi," alisema.

Kwa upande wake, Mbunge wa Bukoba Mjini, Stephen Byabato, alifikisha kwa Makonda changamoto za ujenzi wa Soko Kuu Bukoba akiomba Chama kiwasaidie.

"Kuna ujenzi wa Soko Kuu la Bukoba na kingo za Mto Kanoni bado upo taratibu, haya tumeshawasilisha Serikali tunaomba Rais Samia atusaidie ili kusonga mbele," alisema Byabato ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Mashariki.

Baada ya maelezo hayo, Makonda alimpigia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tamisemi), Mohamed Mchengerwa, akimpa miezi mitatu kukanyaga Kagera kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo.

Hata hivyo, katika majibu yake Mchengerwa amemuahidi Makonda kwenda Kagera, Desemba mwaka jana.

Utelezaji wa maagizo ya Makonda mkoani Mwanza yameshuhudia kwa Mkuu wa Mkoa huo Amos Makalla juzi kumkabidhi Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Geofrey Pinda, kitabu cha ushughulikiaji kero alioufanya katika kila wilaya mkoani humo.

Aidha, Naibu Waziri Pinda alizindua Kliniki ya Ardhi kwenye viwanja vya Nyamagana jijini humo itakayodumu kwa juma moja kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Mkoani Mara, Mkuu wa Mkoa huo, Said Mohamed Mtanda, ameanza kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Makonda kwa kuhakikisha pikipiki zilizokamatwa na Jeshi la Polisi katika mji wa Sirari, mpakani na nchi ya Kenya zinaachiwa na kukabidhiwa kwa wamiliki husika baada ya kutimiza masharti ya kisheria.

Aidha Makonda alimwagiza RC Mtanda kushughulikia utatuzi wa migogoro ya ardhi inayoelezwa kukithiri katika mkoa wa Mara.

Waziri Mchengerwa alimsimamisha kazi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Pangani mkoani Tanga akidaiwa kushindwa kutekeleza majukumu yake.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda akiwa katika moja ya ziara zake mikoani. Picha na Maktaba.

# Samia kamili kumtua mama ndoo kichwani

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imetenga zaidi ya Sh. bilioni 2.238 kutekeleza miradi mitano ya maji Halmashauri ya Manispaa ya Songea katika mwaka wa fedha wa 2022/23.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA), Mhandisi Patrick Kibasa, alisema hadi sasa fedha ambazo zimeidhinishwa kutekeleza miradi hiyo ni zaidi ya Sh. bilioni 1.37.

Alisema kati ya fedha hizo, serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 145 kutekeleza mradi wa maji wa kimkakati wa miji 28 ukiwemo mji wa Songea na kwamba mradi huo umeanza kutekelezwa tangu Januari, mwaka huu.

Aliitaja miradi mingine inayotekelezwa katika Manispaa ya Songea kuwa ni ujenzi wa mradi wa maji katika Kata ya Subira ambao umeidhinishiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.17 na kwamba mradi umetekelezwa kwa zaidi ya asilimia 40.

Kwa mujibu wa SOUWASA,



serikali imeidhinisha zaidi ya Sh. milioni 322 kutekeleza mradi wa maboresho ya uzalishaji maji katika mji wa Mbinga ambapo mradi umetelezwa kwa asilimia 100.

Miradi mingine ambayo imekamilika kwa asilimia 100 ni wa upanuzi wa mtandao wa maji safi katika mji wa Tunduru.

Alisema serikali imeidhinisha zaidi ya Sh. milioni 355 na mradi wa maji eneo la viwanda Kata ya Lilambo katika Manispaa ya Songea ambapo serikali imeidhinisha zaidi ya Sh. milioni 415.

"Katika Manispaa ya Songea hadi kufikia mwaka 2023, wakazi 260,733 wanapata huduma ya maji sawa na asilimia 88.0, huku mahitaji ya maji katika Manispaa ya Songea ni wastani wa lita milioni 20.593 kwa siku," alisema.

Hata hivyo, alisema mwaka 2023 katika maeneo ya Manispaa ya Songea, uzalishaji wa maji ghafi ni wastani wa mita za ujazo 9,170 kwa siku na kwamba jumla ya maunganisho ya maji safi ni 22,465 ambapo upatikanaji wa huduma ya maji safi ni saa 23.15 kwa siku.

# Siku ya Wanawake Duniani yaacha neema kwa mwanafunzi

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

KILELE cha Siku ya Wanawake Duniani Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, kimeacha tabasamu kwa mwanafunzi mlemavu, Aisha Hassan Swalehe, baada ya wanawake kumchangia Sh. milioni moja.

Harambee ya kumchangia Aisha (16), mwanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Likunja iliongozwa na mgeni rasmi, Mhandisi Zuhura Rashidi aliyemwakilisha Katibu Tawala wa Wilaya ya Ruangwa (DAS), Zuwena Omari.

Mhandisi Zuhura alisema maadhimisho hayo yamefana zaidi kwa sababu yamelenga kuikumbusha jamii hasa wanawake kujitoa kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum na kujikwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadalizi ya maadhimisho hayo, Sada Chonya, alisema kitu muhimu kwa wanawake ni kuendeleza mioyo ya kujitoa na kushikamana na serikali katika shughuli mbalimbali za maendeleo ili kwa pamoja kujenga Taifa.

"Kama kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inavyosema "Wekeza kwa wanawake kuharakisha maendeleo ya Taifa na Ustawi wa Jamii,"

Ni jukumu letu wote kuhakikisha jamii inastawi kupitia kwetu," alisema.

Mgeni rasmi pia alikutana na wajasiriamali pamoja na wataalam kutoka Idara ya Afya kitengo cha Ukimwi na Saratani ya Shingo ya kizazi kisha akashiriki katika zoezi la kupima afya.

Katika hatua nyingine, Diwani wa Kata ya Likunja, Issa Ngongonda, ameishukuru kamati ya maandalizi ya sherehe hizo kwa kuratibu vizuri na kutoa rai kwa wanawake kujiweka karibu na taasisi za kifedha ili kupata mikopo itakayosaidia kuboresha maisha yao.

Wadau wengine walioshiriki maadhimisho hayo ni benki ya NMB iliyokuja na kauli mbiu 'teleza kidigitali' na CRDB iliyoibuka na kauli mbiu ya Wekeza kwa Mwanamke.'






# Wasimamizi kesi za watoto wafundwa

**Na Mwandishi Wetu, Kigoma**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Kigoma, imewataka wasimamizi wa kesi za watoto kuzingatia haki za mtoto kulingana na sheria na mikataba ya kimataifa inayolinda haki zao wanaposhughulikia kesi zao.

Jaji Mfawidhi wa Kanda ya Kigoma, Augustine Rwizile, alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya siku tano kwa washiriki 64 wakiwamo wadau walio mstari wa mbele katika kushughulikia kesi za watoto.

Mafunzo hayo yanahusisha mahakimu wa mahakama za wilaya, waendesha mashitaka, maafisa ustawi wa jamii na wasaidizi wa sheria kutoka taasisi mbalimbali mkoani hapa.

Alisema uendeshaji wa kesi za watoto ni wa tofauti kubwa ikilinganishwa na kesi nyingine.

> **Mafunzo hayo yanahusisha mahakimu wa mahakama za wilaya, waendesha mashitaka, maafisa ustawi wa jamii na wasaidizi wa sheria kutoka taasisi mbalimbali mkoani hapa**

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

HII NI KERO

## Tudhibiti makelele mitaani

Baadhi ya mitaa ikiwemo Temeke Maganga bado kuna matukio yanayosababisha kelele na kuondoa utulivu majumbani.

Katika mtaa huu wa Maganga maeneo ya Kwa Bi Hafasa, kila wikiendi kuna nyumba kunapigwa mnanda ambao huondoa utulivu mtaani. Mnanda pia hukaribisha vijana wahuni na wezi. Wahusika wawalazimishe wahusika kupeleka starehe zao kwenye kumbi maalumu badala ya wazi ambayo huvutia watoto.






MAONI YA MHARIRI

## Kufunga kamera kwenye majiji hakika itasaidia kupunguza uhalifu

KATIKA toleo letu la leo ukurasa wa pili, kuna habari yenye kichwa cha habari `Majiji matano kufungwa kamera kudhibiti uhalifu.'

Habari hii imeeleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imepanga kufunga kamera maalum mikoa yote nchini.

Imeelezwa kwamba kwa kuanzia, kamera hizo zitafungwa katika majiji matano, lengo kubwa likiwa ni kudhibiti matukio ya uhalifu, ujambazi, wizi na ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliyasema hayo baada ya kukutana na Kikosi Kazi cha Miji Salama kinachoratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa ufungaji wa kamera za kuzuia uhalifu.

Waziri Masauni alifafanua kuwa kwa kuanzia, kamera hizo zitafungwa katika majiji matano na kuyataja baadhi yake kuwa ni pamoja na Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza na Arusha.

Hata hivyo, alisema lengo la serikali ni kufungan kamera za namna hiyo katika mikoa yote nchini kwa siku zijazo.

Alisema kuna maeneo ambayo yanatakiwa yawe na udhibiti wa uhalifu hasa kwa kutumia teknolojia na baadhi ya nchi tayari wana mfumo huo na wameanza kufanikiwa kudhibiti uhalifu na makosa ya ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani.

Sisi UELEKEO, tunaamini kwamba teknolojia hii mpya, itasaidia kwa kiwango kikubwa kudhibiti matukio mbalimbali ya uhalifu ambayo hufanywa na watu ama makundi ya watu.

Yamekuwepo matukio mbalimbali ya uhalifu katika miji na majiji yetu ambayo wakati umefika sasa teknolojia ya kisasa itumike katika kuwabaini watu wanaohusika kufanya uhalifu huo.

Nchi nyingi za wenzetu, tayari zinatumia teknolojia hiyo sisi pengine tumechelewa.

Hata hivyo, kila safari, ni hatua nasi ndiyo kwanza tumeanza hatua ya safari yetu na hapana shaka tutafika tu kutokana na dhamira ya serikali yetu.

Yapo matukio hata ya baadhi ya watu kukiuka sheria za usalama barabarani, jambo ambalo kama kamera hizo zitafungwa kila kona ya miji na majiji, hapana shaka madereva watakuwa makini.

Kwa mantiki hiyo, tuwaombe wajumbe wa kikosi kazi wanaosimamia mradi huo, kuhakikisha kwamba wanaupitia vizuri mkataba wa ufungaji wa kamera hizo ili zilete tija kwa Taifa.


## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000

**Mhariri wa Habari:** +255753333330

**Mhariri Michezo:** +255787559090

**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825

**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam

**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro

**Jengo la:** Aura Mall

**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532

**Email:** uelekeohabari@gmail.com


Na Hamisi Kibari

JICHO LANGU

## Tuiunge mkono Wizara ya Elimu maboresho ya mitaala

WIKI iliyopita Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ilifanya mazungumzo na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini, suala kubwa likiwa kuwapa taarifa kuhusu maboresho ya sera ya elimu na mabadiliko ya mitaala.

Hili lilikuwa jambo jema kwa sababu wahariri kwenye vyumba vyao vya habari wakielewa jambo vizuri, basi pia hulitendea haki vyema zaidi pale linapoletwa mezani na waandishi wao.

Hakuna ubishi kwamba yalikuwa na mazungumzo yenye tija ambayo ungetamani kila Mtanzania afahamu namna ambavyo Wizara inakwenda kuboresha mfumo wetu wa elimu.

Kwanza nimpongeze Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwani maboresho haya ya sera na mitaala ya elimu nchini yanatokana na maono yake.

Rais Samia anataka kuona mfumo wa elimu yetu, pamoja na kutoa vijana wenye uelewa wa masomo kama Hesabu, Fizikia, Baolojia, Jiografia na kadhalika lakini pia wawe na uelewa wa baadhi ya vitu kiasi kwamba wanaweza kujiajiri au kuajirika hata baada ya kuhitimu masomo ya kidato cha nne.

Kwa mujibu wa mtaala mpya kutakuwa na mkondo wa masomo ya jumla kama ilivyo sasa na mkondo wa masomo ya amali. Mkondo wa Elimu ya Amali umegawanyika katika michepuo ya fani za kilimo na ufugaji, umakenika, sanaa bunifu, michezo, ufugaji wa nyuki, urembo, n.k.

Mbali na masomo hayo mwanafunzi pia atasoma masomo ya Hisabati, Elimu ya Biashara, Kingereza na Historia ya Tanzania pamoja na Maadili ili kupata stadi za msingi katika mawasiliano, stadi za maisha na uzalendo.

Somo la ujasiriamali ambalo kwa sasa Wizara iko katika mchakato wa kufundisha walimu, wahariri waliambiwa kwamba litakuwa linafundishwa kwa wanafunzi wa mikondo yote.

> **Somo la ujasiriamali ambalo kwa sasa Wizara iko katika mchakato wa kufundisha walimu, wahariri waliambiwa kwamba litakuwa linafundishwa kwa wanafunzi wa mikondo yote.**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda aliwaambia wahariri kwamba shule za sekondari zinazofundisha mafunzo ya amali kama unavyoelekeza mtaala mpya, zitakuwa zinaongezeka kidogokidogo kadri shule zitakavyokuwa zinajiimarisha kwenye vifaa na walimu.

Alisema kwamba kwa sasa shule za serikali zilizoanza kutoa mafunzo ya amali ni 26 na za binafsi ni 68.

Akafafanua kwamba hata shule zote zilizoanza kutoa mafunzo ya amali, serikali kupitia taasisi zake ilijiridhisha kuwepo kwa zana na nyenzo za kufundishia pamoja na walimu wa fani husika.

Alisema Sera ya Elimu iliyofanyiwa maboresho inasisitiza suala la 'elimu bila ukomo' na hivyo walimu pia watakuwa wanapata mafunzo ya mara kwa mara ili kunoa uwezo wao na kuwawezesha kwenda na wakati.


Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dkt. Aneth Komba alisema mafunzo kwa ajili ya utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa yametolewa kwa walimu kuanzia wa elimu ya awali, maofisa elimu na wadhibiti ubora.

Naye Mkurugenzi wa Elimu ya Juu, Profesa Peter Msofe alisema shughuli ya uandaaji wa walimu watakaofundidha walimu wenzao juu ya mitaala mipya inaendelea na pia itakuwa endelevu.

Hayo ni machache sana kati ya mengi mazuri yaliyomo kwenye mabadiliko ya sera ya elimu na maboresho ya mitaala.

Hivyo ni vyema kila Mtanzania kwa nafasi yake aunge mkono maboresho haya na kuhakikisha yanafanikiwa na anayetaka kujua mengi afuatilie kwenye tovuti ya Wizara.

Kinachoonekana kwangu ni kwamba mitaala mipya siyo tu itasaidia kufuta ujinga bali na kusaidia katika mapambano dhidi ya adui umaskini.



# A. Kusini yaendelea kumuenzi Nyerere

**Na Mwandishi Maalum**

SERIKALI ya Afrika Kusini, imeendelea kutambua na kuuenzi mchango wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika harakati za kupigania uhuru wa nchi hiyo na Bara la Afrika kwa ujumla.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Afrika Kusini, Candith Mashego-Dlamini, aliyasema hayo wakati akichangia hoja katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri la SADC uliomalizika Machi 11, mwaka huu jijini Luanda, Angola.

Akizungumza kwenye agenda ya sanamu ya Hayati Mwalimu Julius Nyerere iliyozinduliwa rasmi Februari 18, mwaka huu jijini Addis Ababa, Ethiopia, Dlamini alieleza kuwa uzinduzi wa sanamu hiyo ni ishara muhimu ya kuenzi jitihada na mawazo yake ambayo yataendelea kukumbukwa daima.

Aidha, alieleza kuwa Tanzania kupitia Mwalimu Nyerere iliweka bayana nia ya dhati na ya wazi ya kuzikomboa nchi za Kusini mwa Afrika ikiwemo Afrika Kusini.

Alisema katika mapambano hayo ilitoa usaidizi wa kisiasa, mawazo, vifaa, hifadhi kwa viongozi na wapiganaji wake ikiwemo African National Congress (ANC) na Pan-African National Congress hadi pale walipofanikisha upatikanaji wa Uhuru wa Afrika Kusini mwaka 1994.

Tanzania ndiyo ilikuwa kimbilio la kwanza kwa Afrika Kusini baada ya kutokea kwa mauaji maarufu ya 'Sharpeville massacre' yaliyotokea Machi, 21,mwaka 1960.

"Hatua hii ikaongeza chachu ya Mwalimu Nyerere kuendeleza juhudi za kupinga ubaguzi wa rangi na ukoloni kwa ujumla wake na hivyo kujidhatiti kufanikisha kupatikana kwa uhuru kamili wa Afrika nzima," alisema.

Alisema jitihada hizo zilipelekea kuanzishwa kwa Muungano wa nchi za Afrika (OAU) mwaka 1963 na baadaye kuitwa Umoja wa Afrika (AU) mwaka 2002 pamoja na uanzishwaji wa Kamati ya Ukombozi ya OAU jijini Dar es Salaam.

Alisema kama hiyo ilitoa misaada ya kifedha na vifaa katika kuchagiza harakati za ukombozi wa nchi za bara la Afrika zilizokuwa chini ya utawala wa kikoloni wakati huo Mwalimu Nyerere akiwa miongoni mwa walezi wake.

Kwa upande wa SADC, Dlamini alimwelezea Mwl. Nyerere kuwa ni miongoni mwa viongozi waanzilishi wa SADCC mnamo mwaka 1980 na baadae SADC ambayo chimbuko lake lilianzia kwenye nchi zilizokuwa Mstari wa Mbele katika kupinga ubaguzi wa rangi uliokuwa ukiendelea Afrika Kusini na nchi nyingine za kusini mwa Afrika.

Pamoja na hayo, ameongeza kuwa Serikali ya Afrika Kusini na wananchi wake itaendelea kuenzi mchango thabiti wa Mwalimu Nyerere ambaye wakati wote hakusita kupaza sauti kupinga vitendo vya kikatili na ubaguzi dhidi ya wananchi barani Afrika na dunia nzima.

# OSHA yakamilisha tathmini ya awali JNHP

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), umekamilisha tathmini ya awali ya vihatarishi vya usalama na afya katika eneo la mradi wa kuzalisha umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHP).

Taarifa ya kukamilika kwa zoezi la tathmini ya vihatarishi imetolewa na Mtendaji Mkuu wa OSHA ambaye pia ni Mkaguzi Mkuu wa maeneo ya kazi nchini, Khadija Mwenda, alipofanya ziara katika eneo la mradi hivi karibuni kama sehemu ya kukamilisha kazi hiyo ya tathmini.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 60 cha Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003, wamiliki/wasimamizi wa sehemu za kazi wanawajibika kuhakikisha kwamba maeneo yao ya kazi yanafanyiwa tathmini ya vihatarishi vya usalama na afya walau mara moja kwa mwaka ili kupata taarifa muhimu zinazohitajika katika kuandaa mikakati madhubuti ya kulinda uwekezaji na kuwakinga wafanyakazi dhidi ya athari za vihatarishi katika eneo la kazi husika.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Khadija, alisema:

"Ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa matakwa ya sheria tajwa, mwaka 2022, Shirika la Umeme (Tanesco) kwa kuzingatia uzoefu wetu na uwepo wa wataalam wa kutosha waliobobea katika masuala ya usalama na afya kazini, lilituomba kufanya tathmini ya awali ya vihatarishi katika eneo la mradi na kutoa ushauri elekezi kuhusiana na uimarishaji wa mifumo ya kudhibiti vihatarishi mahali pa kazi.

"Hivyo, baada ya wataalam kukamilisha kazi niliyowatuma nami nimeona ni muhimu kufika katika eneo la mradi kuona kama kazi hiyo imefanyika kikamilifu. Aidha, imekuwa ni muhimu pia kuja kuona hali ilivyo baada ya mtambo mmoja kuwashwa kwani wakati tathmini inafanyika uzalishaji ulikuwa bado haujaanza," alisema.

Aidha, alimshukuru na kumpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan pamoja na viongozi wote waandamizi wa serikali kwa kuwa na dhamira ya dhati ya kutekeleza mradi huo wa pili kwa ukubwa Barani Afrika ambao ni dhahiri kuwa utamaliza changamoto ya upungufu wa nishati ya umeme nchini pindi utakapokamilika.

"Hatua iliyochukuliwa na serikali yetu kutekeleza mradi huu wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji ni ya msingi sana na yenye tija kubwa katika kuchagiza ukuaji wa uchumi hapa nchini," alisema.

Akielezea mchango wa OSHA katika mradi huo, Kiongozi huyo amebainisha kuwa Taasisi yake imekuwa ikifanya ukaguzi wa usalama na afya mara kwa mara tangu mradi ulipoanza na hivyo kupunguza ajali, magonjwa na vifo miongoni wa wafanyakazi wa mradi.

Aliongeza kuwa kaguzi, miongozo na ushauri ambao umekuwa ukitolewa na wataalam wa OSHA umesaidia kwa kiwango kikubwa mradi huo kutekelezwa kwa mafanikio ikiwemo kukamilika kwa wakati na katika viwango stahiki kutokana na kuwa na nguvukazi yenye afya njema pamoja na zana na mitambo yenye ufanisi wa kutosha.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Mradi huo kutoka TANESCO, Mhandisi Mathew Bundala, ameushukuru uongozi wa OSHA kwa ushirikiano wao katika usimamizi wa masuala ya usalama na afya kwa wafanyakazi katika mradi huo jambo ambalo limesaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza ajali, magonjwa na vifo vya wafanyakazi katika eneo la mradi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, OSHA itaendelea kufanya ukaguzi wa usalama na afya katika eneo la Bwawa hata baada ya shughuli za ujenzi kukamilika ili kuhakikisha kwamba uzalishaji unakuwa endelevu na nguvukazi iliyopo inalindwa.



**Mtendaji Mkuu wa OSHA ambaye pia ni Mkaguzi Mkuu wa maeneo ya kazi nchini, Khadija Mwenda.**



# Maajabu ya Tembo pindi wanapokufa watoto wao

**Na Mwandishi Wetu**

WANADAMU siyo viumbe hai pekee ambao wana matambiko ya kushughulikia kifo.

Wanyama wengine pia huonesha tabia pindi mmoja wao anapokufa.

Mfano wa hawa ni tembo wa Asia na kutokana na utafiti mpya,ibada hizi zilipigwa picha kwa mara ya kwanza.

Ugunduzi huo pia unaonesha kuwa tembo hubeba maiti za watoto wao kwa siku kadhaa hadi wapate mahali pazuri pa kuzikia, huku wakitoa vilio kutoka kwenye mikonga yao.

Katika utafiti uliofanywa kati ya mwaka 2022 na mwaka jana, Akashdeep Roy, wa Taasisi ya Elimu ya Sayansi na Utafiti huko Pune na Parveen Kaswan wa Huduma ya Misitu ya India, alipata matukio matano ya kuzikwa kwa watoto wa tembo.

Matukio hayo yalirekodiwa huko Bengal, Kaskazini Mashariki mwa nchi na kwa mujibu wa wanasayansi, hakuna wanadamu waliohusika.

Mazishi ya watoto wachanga, ni matukio adimu sana katika maumbile," Roy aliliambia Jarida la New Scientist.

Nyayo na kinyesi vilivyoachwa njiani ambavyo watafiti walivipata kwenye makaburi matano, viinaonesha kuwa tembo wa rika zote, walichangia kila maziko.

Hii, kwa mujibu wa ripoti, ni ushahidi wa tabia ya huruma na msaada iliyooneshwa na washiriki.

Maiti zote zilipatikana katika nafasi sawa, zikiwa zimezikwa kwenye mifereji ya maji iliyofunguliwa na wakulima na kufunikwa na ardhi na miguu yao juu.

"Ni nafasi inayofikika zaidi ya kushikilia na kuweka maiti kwenye mitaro," Roy alielezea tovuti ya Live Science Portal.

"Nafasi hii pia inaruhusu zaidi ya mwanachama mmoja kushiriki katika mchakato wa mazishi."

Baada ya maziko, wakulima waliohojiwa walidai kuwa walisikia tembo wakipiga tarumbeta kwa mikonga yao.

Roy anaamini kwamba sauti hizi zilionesha uchungu na

>>>Inaendelea Uk. 15



Leo yetu ndiyo kesho yetu
Uelekeo
JARIDA
Jungu Kuu
| Jumatano Machi 13 - 19, 2024 |
JAMII
UCHUMI
SIASA
Jarida hili haliuzwi

# Tunavunja Shirika la Elimu Kibaha badala ya kuanzisha mengine?

UK. 12 & 13



Wanafunzi wa Shule ya Awali iliyo chini ya Shirika la Elimu Kibaha

# Waliosemwa wamechoka 2013, bado wapo Chadema - 8

LEO tunaingia sehemu ya 8 tukiendelea kujikumbusha yaliyokuwemo kwenye waraka wa Mkakati wa Kudai Mabadiliko ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Huu ni waraka uliosambaa mitandaoni mwaka 2013 na kusababisha baadhi ya viongozi waandamizi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) waliotuhumiwa kuandaa mkakati huo kuondolewa.

Baadhi ya mambo ambayo tumeangalia ni namna viongozi wa sasa walioingia madarakani 2004, walivyolalamikiwa kwa kuwa wazito kung'atuka madarakani na kupisha damu mpya, kufanya ubadhirifu, pia walidaiwa kutumia mbinu za maandamano na harakati nyingine kama Movement For Change (M4C) ambazo hata hivyo kwa majibu wa waliokuwa wakitaka mabadiliko, hazikuzaa matunda ya maana.

Tukaona kwamba licha ya mbinu hizo, Chadema hakikufanya vizuri katika chaguzi kubwa na ndogo katika kipindi cha uongozi wa viongozi hao hadi wakati waraka wa mabadiliko unaandikwa.

Waraka huo wa Mabadiliko ulipendekeza Zitto Kabwe ndiye achukue uongozi Chadema (ingawa hatajwi kwa jina) lakini kabla wataarishaji wa 'mapinduzi' hawajakaa sawa mambo 'yakabumbulika', wakafukuzwa, Zitto akaanzisha ACT - Wazalendo.

Pia tuliangalia vikwazo ambavyo waandaaji wa mkakati huo wa mabadiliko walikuwa wakiviona mbele yao.

Baadhi ya vikwazo hivyo walisema ni pamoja na mshindani wao mkuu (Freeman Mbowe), kuonekana hana mpago wa kuachia madaraka na kuna watu wanaomuunga mkono na wengine kuwa na hofu kwamba akitoka madarakani chama kinaweza kuyumba na kwamba mtu wanayemtaka (Zitto Kabwe) amekuwa akifanyiwa propaganda chafu.

Halikadhalika tuliangalia jinsi walivyokuwa wamepanga mtandao wao wa ushindi.

Wiki iliyopita tunaangalia namna walivyokuwa wamejipanga kufanikisha mpango wao wa kufanya mapinduzi baridi ndani ya Chadema lakini ikashindikana.

**MAPENDEKEZO MAHSUSI NA HITIMISHO**

Katika kuhitimisha tunapendekeza mambo mahsusi yafuatayo:

Kuhusu Bajeti: Tunapendekeza kwamba bajeti ya mkakati huu isipangwe hivi sasa. Ni muhimu tu sote kuelewa kwamba wakati wenzetu wanatumia raslimali za taasisi kujijenga na kutekeleza mkakati wao wa ushindi, sisi tunapaswa kuingia mifukoni. Kwa kila kila mmoja wetu atakuwa budget conscious ili kuepuka matumizi makubwa ya pesa.

Hata hivyo, kwa kuzingatia kwamba lazima pesa inahitajika ni muhimu M1 na MM (Mhusika Mkuu kwa maana ya Zitto) kujaribu kuangalia namna ya kuraise pesa na kushauri.

Otherwise, tutakapokuwa tunahitaji kufanya hatua yoyote ama jambo lolote tutakuwa ndo tunapiga hesabu za funds tunazohitaji kwa jambo husika na kuingia katika utekelezaji.

Kuhusu mwenendo wa MM kuanzia sasa:

Ni maoni yetu pia kwamba kuanzia sasa MM aenende katika mwenendo ambao utarahisisha ushindi. Mfano tunapendekeza afanye yafuatayo kuanzia sasa:

Apunguze ukaribu na viongozi wa serikali na wa chama tawala na awe crical zaidi na utendaji wa serikali nje na ndani ya bunge.

Ashiriki kikamilifu katika shughuli za taasisi yetu zikiwamo vikao vyote vinavyomhusu, operesheni mbalimbali, chaguzi ndogo, nk.

Aendelee kushusha 'nondo' ndani ya chombo chetu cha uwakilishi na kuendelea kuwa juu ya wawakilishi wengine katika hoja mbalimbali zenye maslahi ya kitaifa.

Ajitahidi kudhibiti jazba hata pale anapokuwa amebambikiziwa tuhuma nzito namna gani. Atulie, ashauriane na wazee ili kuona namna nzuri ya kujibu tuhuma zinazomkera. Tukumbuke kwamba wakati mwingine kukaa kimya ni jibu zuri zaidi kuliko hoja nzito.

Sambamba na 'iv' hapo juu, adhibiti sana emotion ili kuhakikisha kila kitu kinachofanywa ama kuzungumzwa kinachomgusa asikimbilie kuongea na vyombo vya habari ama kwenye mitandao ya kijamii bali afuate kile tulichokizungumza kwenye kipengele cha 'iv' hapo juu.

Kuhusu mapambano ya kuchafuana kwenye mitandao ya kijamii:

Katika hili sisi hatukuona haja ya kufanya hivyo kwa sababu mbili:

Imani yetu kwamba taasisi yetu ni kubwa kuliko watu kwa hiyo ni muhimu kuzingatia kwamba hatuiui taasisi katika mapambano haya. Tukiendekeza mashambulizi kwa njia ya mitandao ya kijamii hatutakuwa na ngao ya kuwakinga watu wa kawaida (wanataasisi na wasio wanataasisi) dhidi ya kujikuta wakiamini kwamba taasisi hii nayo haina jipya ni sawa tu na ile tunayotaka kuitoa.

Tutakuwa tumeiua taasisi na mkakati huu hautakuwa na maana sana kama lengo ni kufanya mabadiliko ya uongozi wa taasisi tu lakini malengo ya taasisi ya mwaka 2015 yasitimie!

Kujikita kwenye mashambulizi kupitia mitandao ni kuzidi kuwashtua wakuu waliopo kwamba bado tuko serious na mkakati wa kuwatoa na kuwafanya wafanye kazi zaidi huku wakiendelea kumpaka matope MM kwamba ndiye anayerusha makombora hayo kwenye mitandao kwa kusudi la kuhujumu taasisi maana hiyo ndo lugha yao.

Hatukatai kwamba wakuu wanajua kabisa kwamba bado MM ana nia ya kumvaa mkuu aliyepo lakini tunajua kwamba kwa sasa wanaamini wamemdhoofisha na hana madhara tena. Ndiyo maana tunataka kutekeleza mkakati wetu kwa siri sana ili wafikiri MM amekata tamaa kumbe ndo anakuja na mkakati mzito zaidi.

Hata hivyo, ni muhimu kukumbushana kwamba wenzetu hawatanyamaza kwa sababu eti sisi tumeacha kuwashambulia kwenye mitandao ya kijamii.

Lazima wataendelea! Wataendelea kumchafua MM kwa kupitia wapuuzi kama yule kichaa wa 'ars' na kundi lake. Nini tutakuwa tunakifanya sasa?

Tutahakikisha tuko busy kupost mambo mema na mazuri yatakayokuwa yakifanywa na MM kila wakati na kuzidi kusambaza sifa zake njema kila inapotokea nafasi. Atakayefanya kazi hiyo ni sisi wengine wala si yeye!

Pia tutahakikisha kila post ya kumchafua inapatiwa majibu bila kutumia ID yake inayojulikana. Ni vema aidha akatupatia majibu na sisi kuyapost ama afungue ID mpya kabisa ambazo hazijawahi kuwepo kwenye mitandao halafu ndo awe anazitumia kujibu lakini kwa kuzingatia tuliyokwishayazungumza hapo juu yaani kutofanya kwa emotion na kuepuka jazba lakini pia kushauriana na watu wa karibu kabla ya kutoa majibu kwa jambo lolote linalomhusu.

Kuhusu kamati ya kitaifa (husussani M2 & M3):

Tulikubaliana kwa kauli moja kwamba katika kutekeleza mkakati huu tunahitaji members hawa wawe wametulia kimaisha. Inakuwa vigumu kwa mfano kumtaka member aende mahali fulani kwa makusudi ya mkakati huu wakati hajui familia yake nyumbani anaiacha inakula nini.

Tuliona kwamba M3 tayari hana kazi kwa sasa tena kwa kufanyiziwa na wakuu waliopo. Ni katika mwendelezo huo huo tunamwona M2 naye akiwa ukingoni kupigwa nje na kuachwa mtupu na wakuu waliopo katika kile wanachokiita wao reshuffle ya ofisi kuu.

Kwa sababu hiyo tukapendekeza kwamba MM kwa kushirikiana na M1 kwa hatua ya kwanza wanaweza kutafuta kiasi cha sh. 2m kila mmoja tukijua kwamba kama members hawa wawili wakisaidiwa milioni mbili mbili wanaweza kuanzisha projects ambazo zitawasustain hata kama hawana ajira. Kwa hatua ya baadaye tutasaidiana kuona kama hawa members wanaweza kusecure good employments mahali, provided hazitawazuia kufanya siasa.



# Vitu vya kula au kuepuka mfungaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAISLAMU nchini wako katika Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ikiwa ni sehemu ya kutekeleza moja ya nguzo muhimu za dini hiyo.

Katika kipindi hiki cha toba, Waislamu walio katika mfungo wanajinyima na kujizuia katika mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kula na kunywa hadi linapozama jua.

Pamoja na hayo, wanaanza safari na juhudi mpya zaidi za kuacha mambo machafu na yale yanayokatazwa katika dini hiyo ili mfungo wao uwe na umuhimu kwa kila muumini.

Mwenyezi Mungu katika Kurani anasema: "Enyi mlioamini! Mmelazimishwa kufunga kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu." (2:183).

Hapa Waislamu wote wanalazimishwa kufunga isipokuwa wale wenye udhuru kama wagonjwa, wasafiri na wanawake walio kwenye hedhi.

**TAHADHARI YA KUJAZA TUMBO**

Swahaba mmoja Al-Miqdam ibn Ma'diy-karib kasimulia: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema, 'Hajawahi mwanadamu kujaza vibaya chombo chochote kama anavyolijaza tumbo lake. Yanamtosha mwanadamu matonge kadhaa ya kunyoosha mgongo wake.

Lakini ikibidi, basi theluthi moja (ya tumbo) iwe kwa ajili ya chakula, theluthi moja iwe kwa ajili ya maji na theluthi moja iwe kwa ajili ya pumzi." (Imepokwa na Ahmad na Tirmidhi).

Kwa mujibu wa uchunguzi, katika mwezi huu, wengi waliofunga huitumia nafasi hii kupika mapochopocho au aina nyingi za vyakula wakati wa kufuturu pale jua linapozama, bila kuangalia athari zake kiafya au kuzingatia mafundisho ya dini.

Kwa mfano, unakuta mtu amepika mihogo kwa nazi, chapati, vitumbua, magimbi na uji.

Kimsingi ukiviangalia vyakula vyote hivi, unagundua ni vyakula vya wanga na humwoni mtu huyu akiwa na mpango wowote wa kula mboga za majani wala matunda.

Mara nyingi hali hii huwafanya wengine kesho yake kujawa na gesi tumboni hali inayozorotesha utendaji kazi wake.

Mtu wa aina hiyo mara nyingine katika kipindi hiki cha Mwezi wa Ramadhani, hujikuta anaongezeka uzito na hata anavimbiwa kiasi cha kushindwa kufanya ibada za usiku ambazo ndizo muhimu sana kufanywa katika mwezi huu mtukufu.

**KUFUNGA KWA AFYA**

Ipo hadithi ambayo wengine wanahofu na usahihi wake lakini amekaririwa Mtume Muhammad (SAW) akisema: Fungeni mpate siha nzuri."

Madaktari takrbani wote wanathibitisha faida ya kufunga kwa ajili ya afya, hususani asiyejaza tumbo hadi sehemu ya hewa na maji.

Imam Ja'far As-sadiq (a.s.) asema, "Kila kitu kina utakaso, na kitakaso cha mwili ni kufunga (saumu)."

Dk Abdul Aziz bin Ismail alikaririwa akisema kwamba kufunga siku moja ni kinga ya maradhi ya mwaka na sasa kuna hospitali mbalimbali ambazo zinahimiza na kusisitiza umuhimu wagonjwa wao wao kufunga kwa ajili ya manufaa ya afya zao.

Mwalimu mmoja wa Chuo Kikuu Cairo, Dk Muhammad Dhawahir alipata kusema: "Ugonjwa wa kuzidi maji mwilini, unene, moyo, ini, mapafu moja ya mambo ya kumsaidia mgonjwa ni kujizuia kula (kufunga saumu)."

Katika makala moja iliyoandikwa katika jarida la "New England Medicine", inabainishwa kwamba kula ndani ya saa 6 hadi 8 katika siku na saa ziliyobaki 16-18 kukaa mbali na chakula hukinga mwili kutokana na magonjwa tofauti, ikiwa ni pamoja na kupunguza shinikizo la damu, kiriba tumbo na kurefusha maisha.

Katika makala hiyo imesisitizwa kwamba kufunga kula ni moja ya njia zinazoweza kupendekezwa katika tiba ya kiribatumbo, kisukari na magonjwa ya moyo. Makala hiyo inapendekeza kufunga siku mbili au wiki au kula kiasi kidogo sana kila siku hadi daktari atakapoagiza vinginevyo.

Katika kusisitiza umuhimu wa kufunga, hivi karibuni Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Profesa Mohamed Janabi ambaye ni bingwa wa magonjwa alitoa somo kwenye video ambayo imekuwa ikizunguka kwenye vyombo vya habari akieleza umuhimu wa kufunga kwa ajili ya afya.

Utafiti uliofanywa kwa kutumia binadamu na wanyama umeonyesha kwamba kufunga kila baada ya muda maalumu huuisha upya michakato wa usagaji vyakula katika mwili (metabolism), kitu ambacho hufanya afya ya seli za mwili kuboreka.

**NINI CHA KUFUTURU?**

Katika kuwaongoza waumini wa dini ya Kiislamu kwenye vyakula vinavyofaa kufuturu, Kiongozi wa dini hiyo, Mtume Muhammad (S.A.W) anasema: "Fungueni swaumu zenu kwa tende, au vinginevyo, basi fungueni kwa maji, kwani ni twahara (ni masafi)."

Watafiti na watalaamu wa lishe wanakubaliana kwamba kula tunda hili wanapofungua ni muhimu kwa sababu lina sukari inayomsaidia mfungaji kupata nguvu haraka baada ya siku nzima kubaki tumbo likiwa wazi na kufanya kiwango chake cha sukari mwilini kupungua.

Sukari hii inakwenda kwenye ubongo na kumsaidia mfungaji kuondokana na ulegevu wa siku nzima na pia, hufanya glukosi ya mwili kujisawazisha na kumfanya mtu apate nguvu na nuru zaidi ya macho.

Mfungaji anapopata nguvu na nuru ya macho anakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kufanya ibada.

Tende pia ni chanzo kizuri cha nyuzinyuzi ambazo huwezesha umeng'enyaji wa chakula mwilini kuendelea, huzuia tatizo la kushindikana kwa michakato hiyo ya uyeyushaji wa chakula mwilini.



Vilevile, tende ni chanzo kizuri cha potasiamu, madini ambayo ni muhimu kwa usawazishaji wa maji mwilini.

Mtume (S.A.W) alikuwa na kawaida ya kula tende kwa idadi ya witiri yaani moja, tatu, tano au saba na kuendelea.

Hivyo, wale ambao hawapendelei ladha ya tende wanaweza kupata manufaa ya chakula hiki kwa kula angalau tende moja, na wale wanaopendelea tende, basi wanaweza kula tatu, tano na kuendelea.

Kitu kingine kinachohitajika mwilini kwa mfungaji pindi anapofungua ni maji. Inafahamika maji ndiyo yanayojenga mwili na mtu anaweza kuishi kwa zaidi ya siku kumi kwa kunywa maji tu, hivyo ni kitu muhimu sana mwilini. Watalaamu pia wanaseme sehemu kubwa ya mwili wa mwanadamu ni maji na wanashauri kila siku watu kujenga tabia ya kunywa maji ya kutosha.

Vilevile, wakati wa kufungua, inashauriwa kunywa chai, kahawa au uji ili tumbo na ubongo vipate kitu cha moto kuweza kushitua baada ya siku nzima kudorora. Pia huzuia maumivu ya kichwa.

Hata hivyo, inatakiwa kuepuka unywaji mwingi wa vinywaji hivi, hasa vyenye caffeine kwani husababisha mtu kwenda sana haja ndogo, hivyo maji kupungua kwa kiwango kikubwa mwilini.

Kinywaji kingine muhimu ni maziwa. Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali vya kitaalamu, kinywaji hiki ni chanzo kizuri cha laktosi, madini ya kalsiamu, potasiamu na fosiforasi.

Unaweza kutengeneza juisi ya maziwa ukachaganya na tende na hata kuongeza tunda lingine kama parachichi au ndizi.

Matunda nayo hayatakiwi kukosekana kwa kila mfungaji. Hiki ndicho chanzo cha vitamini na madini kama vile vitamin C, potasiamu, folati, majimaji, sukari na nyuzinyuzi.

Wataalamu wa lishe pia wanashauri vyakula vya jamii ya njugu viliwe kwani ni vyanzo vizuri vya protini, madini ya chuma, vitamin E na mafuta. Vyakula hivyo ni kama korosho, njugu mawe, karanga na lozi (almond).

Unaweza kujiuliza vyakula hivyo vinaliwaje kwani si vyakula vikuu kama mihogo au viazi.

Kwa wanawake, wanaweza kupika njugumawe kwa nazi, vyakula vya sukari wakaweka na lozi, karanga ikatumika mbadala wa nazi kwenye kuunga chakula, biskuti za lkaranga, juisi ya maziwa na tende ikachanganywa na korosho au karanga.

Baada ya kufuturu, familia ikiwa imekaa inasikilizallKurani tukufu ikisubiri kuanza ibada za usiku inaweza kupata korosho, karanga na lozi na kushushia kwa juisi au chai.

Hata hivyo, inatakiwa kuwa makini na kutokula kwa kiwango kikubwa cha vyakula hivi jamii ya njugu kwani kutokana na mafuta yake, husababisha kuongezeka mwili.

Kwa sababu Watanzania wengi wamezoea sana vyakula vya wanga, kipindi hiki ni cha kuwa waangalifu kwani wanga hukaa hutunzwa mwilini kwa njia ya mafuta na kwa sababu wengi wakishafuturu hawafanyi sana kazi ngumu, ni vema kutokula kiwango kikubwa cha wanga.

Wanga husababisha maradhi mengi hasa yasiyoambukiza kama kisukari, magonjwa ya moyo na kiharusi, hivyo si vyakula vya kupendelea sana.

Katika kila mlo wakati wa kufuturu, ni vizuri kula mboga za majani kwani zina faida sana mwilini kutokana na kuwa na virutubisho vingi kwa maana ya madini na vitamini.

Kwa jumla, muumini aliyefunga anapaswa kula vitu vyenye faida mwilini vya makundi yote na kuhakikisha hali chakula kupita kiasi kwani chochote kinachozidi huwa na madhara.

Ikumbukwe kuwa, Ramadhani si mwezi wa kula na kufanya maonesho ya kula, ujuzi wa mapishi wala kula sana, bali mwezi unaopaswa kutumika kwa ibada na kuomba toba kwa Mwenyezi Mungu.

# Tunavunja Shirika la Elimu Kibaha badala ya kuanzisha mengine?



Wanafunzi Shule ya Sekondari Kibaha

**Na Dkt. Felician Kilahama**

Ni vyema na haki kumshukuru Mungu aliye hai ambaye ni mwingi wa rehema pia fadhili zake kwetu ni nyingi.

Shirika la Elimu Kibaha (SEK) ambalo ni zao la ufadhili kutoka mataiafa ya Ulaya Kaskazini yanayojulikana nchi za Nordic (Nordic Countries) ikiwa ni pamoja na: Denmark, Finland, Norway na Sweden, ndilo hasa ninalizungumzia katika makala haya.

Baada ya Tanganyika kupata uhuru Disemba 9, 1961; Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwatangazia wananchi kuwa pamoja na taifa kuwa huru tulikuwa tunakabiliwa na maadui watatu: Ujinga, Umaskini na Maradhi .

Kadhalika, Mwalimu aliongeza kuwa tunayo kazi kubwa ya kufanya" na kufafanua akisema: wakati wananchi katika mataifa yaliyoendelea kiuchumi na kijamii wanatembea; sisi itatulazimu tukimbie tena kwa nguvu na spidi/kasi kubwa ili kujiletea maendelea tunayoyataka .

Kulingana na maono/dira ya kujiletea maendeleo halisi, Baba wa Taifa aliongeza kuwa ili tuweze kusonga mbele ipasavyo, taifa linahitaji kuwa na vitu vine: Ardhi, Watu, Siasa-Safi na Uongozi-Bora .

Kwa mtazamo huo, mataiafa ya Nordic yakawa ya kwanza kuisaidia Tanganyika iweze kupiga hatua katika juhudi zake za kujiletea maendeleo.

Hivyo, mataifa hayo yakaamua kuunga mkono juhudi za taifa kwa kuanzisha Mradi katika eneo la Tumbi, Kibaha (takribani kilomita 30 kutoka Dar es Salaam).



Mradi huo ulijulikana kama: 'Nordic-Tanganyika Project na baadaye kujulikana: Kituo cha Elimu Kibaha (Kibaha Education Center-KEC).

Mradi ulianzishwa mwaka 1963 na kuendeshwa kwa ushirikiano mzuri kati ya nchi za 'Nordic' pamoja na Serikali ya Tanganyika (kabla haijaungana na Zanzibar: kuzaliwa Tanzania Aprili 26, 1964. Mradi ulihusisha mambo muhimu-yafuatayo:

Mosi, Shule ya Msingi Tumbi, kadhalika Shule ya Sekondari Kibaha, kidato cha kwanza hadi cha sita;

Pili, Kituo Cha Afya (Kibaha Health Center KHC);

Tatu, kituo cha Ufugaji Kuku na Uzalishaji Vifaranga wa nyama na mayai (Kibaha Poultry Unit (KPU)

Nne, Kituo cha Ng'ombe wa Maziwa na Uzalishaji Mitamba (Diary Farm Unit);

Tano, Kituo cha Wakulima na Ufundi-Sitadi (Farmers Training Center FTC). Kupitia kituo hicho wakulima wengi (wake kwa waume) kutoka vijiji mbalimbali Mkoani Pwani na kwingineko, waliweza kupata mafunzo ya muda mfupi yaliyohusu shughuli zao za kilimo na ufugaji za kila siku. Isitoshe, walipata mafunzo ya ufundi-sitadi kwa nadharia na vitendo;

Sita, Utawala na Uendeshaji. Hii ilihusisha mambo kadhaa ikiwemo masuala ya: Utawala na Uendeshaji ; Kitengo cha Miliki (Estate Management); Kitengo cha Karakana na Mitambo; Kitengo cha Bohari Kuu na Ugavi (procurement and supplies).

Saba, Vilevile mradi ulihusisha Maktaba kubwa ambayo iliwekwa na Ukumbi mkubwa wa mikutano na masuala mbalimbali ya kijamii.

Kadhalika, kukawekwa mkazo katika Elimu ya Watu Wazima na KEC ilikuwa msitari wa mbele kuhakikisha vijiji vyote vilivyokuwa karibu vikinufaika na elimu ya watu wazima kutokana na wakazi wake kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Niwashukuru na kuwapongeza wananchi wa nchi za Nordic kupitia Serikali zao, kwa moyo wa upendo na kuweza kutoa misaada ya hali na mali kuiwezesha Tanganyika baada ya kupata uhuru, iweze kupiga hatua katika juhudi zake za kupambana na ujinga , umaskini na maradhi .

Shirika la Elimu Kibaha, liliendeshwa na wataalam na kutumia fedha-nyingi kutoka mataifa ya Nordic yaani Denmark, Finland, Norway na Sweden hadi walipokabidhi usimamizi na uendeshaji wake serikalini mwaka 1970.

Tangu 1970 hadi 2024 (takribani miaka 54) siyo muda mfupi isipokuwa najiuliza je, Shirika linavunjwa kwa sababu limetimiza malengo yaliyokusudiwa au kuna sababu nyingine za msingi?

Kimsingi KEC imechangia kuwaletea maendeleo Watanzania wengi kupitia nyanja za elimu, afya, kilimo/ufugaji hasa kuku wa nyama/mayai na maendeleo ya jamii kwa ujumla.



Wanafunzi Shule ya Sekondari Kibaha wakiwa na wanafunzi kutoka nchi ya Sweden, walipowatembelea kwenye ziara ya kimasomo

Kupitia masuala hayo muhimu KEC ikawa imetoa mchango mkubwa katika vita dhidi ya maradhi, ujinga na umaskini.

Kadhalika tangu tupate uhuru ni takribani miaka 62 imepita sasa lakini ukitathimini kwa undani unaona maadui watatu waliotangazwa na Hayati Mwalimu Nyerere baada ya uhuru bado ni changamoto kubwa.

Pamoja na taifa kupiga hatua kwa kiasi kikubwa lakini bado hatujafanikiwa kikamilifu kushinda vita dhidi yao kwa asilimia 100.

Hii inamaana maradhi, ujinga na umaskini' bado ni tatizo. Kama Hayati Mwalimu Nyerere alivyowahi kusema inatupasa kuongeza kasi ili kukimbizana na hao-maadui bila ya kuchoka hadi wametokomezwa kabisa.

Kuvunja Shirika la Elimu Kibaha (SEK) wakati likiwa linahitajika katika kuendeleza vita dhidi ya 'maadui wa Watanzania'; siyo jambo jema kwa mtazamo wangu.

Inawezekana kumekuwepo na mapungufu ya kibinadamu, katika kulisimamia na kuliendesha shirika. Badala ya kuharakisha kulivunja bora tuweke mikakati halisi na madhubuti ya kukabiliana na mapungufu yaliyoainishwa.

Kimsingi Shirika lina manufaa kwa Watanzania wengi, sidhani kama waliotusaidia kuanzisha shirika wanafurahi kuona linavunjwa maana umuhimu wake bado upo.

Kimsingi SEK bado ni chombo muhimu cha kuwaletea maendeleo Watanzania. Kadhalika, kuwepo kwake na kufanya kazi ipasavyo ni mchango mkubwa wa kuwatia moyo walioona umuhimu na kuanzisha chombo hicho takribani miaka 60 iliyopita.

Tusiangalie SEK kama kiwanda cha kutengeneza fedha haraka bali tujali zaidi manufaa yake kwa wengi. Mathalani, elimu inahitaji muda mrefu kufanikisha; vivyohivyo kwa afya na maradhi, mazingira ya kupigana na maadui hao



Majani ya kulisha mifugo yaliyozalishwa na TEK

ni tofauti na kiwanda cha kutengeneza bidhaa kama nguo au sabuni na kupata faida haraka.

Tanzania tujifunze kwa nchi kama China au nchi nyinginezo zenye kujiletea maendeleo ndani ya kipindi kifupi cha miaka 60. Je, ni maamuzi gani yaliyowasaidia hadi kupiga hatua kubwa sana kiuchumi na kijamii? Inawezekana Tanzania katika sera/sheria tunazoziweka tunakumbatia vitu visivyoleta tija.

Wakati wa kipindi cha Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere, taifa liliwekeza sana kwenye uchumi wa viwanda: tukawa na viwanda kadhaa maeneo mbalimbali nchini. Mathalani, kiwanda cha Urafiki kutengeneza nguo hasa kanga na Vlvitenge. Pembeni kukawepo cha kutengeneza bidhaa za kilimo (Urafiki Farm Implements).

Kama taifa la wakulima wa pamba tukaanzisha viwanda kadhaa vya kutumia pamba kutengeneza nguo/bidhaa nyinginezo. Mathalani, Kilitex, Mwatex, Mutex, lakini pia kuwepo viwanda vingine kama Phillips kutengeneza radio (Arusha) na viwanda vya dawa na kusindika vyakula, viwanda vya ngozi pamoja na kutengeneza bia (Tanzania Breweries) na kiwanda cha kuengeneza karatasi kilichopo Mgololo Wilayani Mufindi.

Tukawa na benki zetu na vyama vya ushirka ambavyo vilikuwa na nguvu vikiwahudumia wakulima/wafugaji ipasavyo.

Tuliteleza pale tulipokumbwa na sera ya ubinafsishaji kwa msingi kuwa Watanzania wengi watanufaika na hatua hiyo kiuchumi.

Mpaka sasa ni vigumu kuona matokeo halisi kufuatana na hatuo hiyo maana hali bado ni 'tete' kwa wananchi waliowengi mijini na vijijini isipokuwa wapo wachache wanaochekelea .

Kwa mtazamo wa kijumla, bado maadui ujinga', 'maradhi' na 'umasikini yanavuruga maendeleo kwa Watanzania waliowengi.

Tunapofanya maamuzi ya kimifumo kama kufuta kilichokuwepo tusifanye hivyo kihisia bali tuzingatie halihalisi na matokeo yenye tija kutokana na tafiti za kina.

Tumo tena kwenye mfumo wa uchumi wa viwanda je, tuna uhakika wa kutosha kuwa uwekezaji kiviwanda kupitia sekta binafsi; utakuwa wa manufaa kwa Watanzania wengi au ni kikundi cha watu wachache tu (elite group) watafaidi mema ya nchi?

Ni vema tamko la serikali kufuta KEC lituchangamshe tufikiri kwa kina ikiwa tunayo miaka 62 kibindoni tangu tuwe taifa huru; lakini bado, kwa kiasi kikubwa, tunahangaishwa na maadui haohao watatu: 'Ujinga', 'Maradhi' na 'Umaskini'. Inawezekana ujinga na umaskini vikaungana na kupelekea Watanzania wengi kujikuta katika dimbwi la kuangamiza mustakabli mzima wa maisha yao kwa kukosa MAARIFA .

Tujitathimini tunakosea wapi na tujisahihishe kwa faida ya Watanzania wote, lakini ni vizuri kwa waliokuwa wanufaika kutokana na uwepo wa Shirika la Elimu Kibaha wakajulishwa sababu za msingi zilizosababisha Shirika la Elimu Kibaha kuvunjwa badala ya kuanzusha mashirika mengi ya aina hiyo.

# Namna bora ya kuhifadhi mayai bila kuharibika

**Na Mwandishi Wetu**

MOJA ya miradi ambayo sasa hivi inawasaidia watu wengi kunyanyua kipato chao ni ufugaji wa kuku.

Kuna aina mbalimbali ya kuku wanaofugwa. Kuna kuku wa nyama, kuku wa mayai, kuku wa kienyeji na kuku chotara. Hawa chotara ni pamoja na kuku wanaojulikana kama kroila, saso na waliopewa jina la Malawi ambao mara nyingi huwa ni weusi.

Watu wengi sasa hivi wanapendelea kufuga kuku chotara kutokana na ukweli kwamba wanatabia zinazofanana na kuku wa kienyeji lakini wao wanakuwa kwa haraka kidogo na wana nyama nyingi.

Lakini ndani ya biashara hii ya kuku, kuna biashara ya mayai ambayo ndio makala haya yanaangazia. Kuna watu wanaofuga kuku kwa ajili ya mayai ya kula (layers) lakini pia kuna wanaofuga kuku kwa ajili ya mayai ili kutotolesha vifaranga.

Ukiacha kampuni kubwakubwa ambazo aghalabu huzalisha mayai kwa ajili ya kutotolesha vifaranga wa kuku wa nyama au wa mayai ya kula tu (yasiyo na mbegu kwa maana ya layers), sasa hivi wananchi wengi pia wanajishughulisha na kuzalisha mayai ya kuku chotara.

Kuna ambao kazi ni kuzalisha au kuzalisha na kutotolesha lakini kuna wenye mitambo yao ya kutotoleshea mayai (incubators) ambao hununua mayai kwa wafugaji.

Biashara ya incubators nayo imekuwa maarufu nchini, baadhi zikiagizwa kutoka nje na nyingine zikitengenezwa na baadhi ya vijana wa hapa hapa Tanzania.

Mayai ni bidhaa hafifu na inayoharibika kwa haraka, hivyo ni lazima yashikwe kwa uangalifu na kutunzwa vizuri baada ya kutagwa ili yasivunjike au kuharibika.

Watu wengi wanaonunua mayai kutoka dukani au wanaokwenda kutotolesha watatambua mara moja kuwa mayai hayo yamevunjika au yameoza. Tatizo hili linaweza kutokea kutokana na utunzaji na uhifadhi wakati mayai bado yakiwa kwa mfugaji.

Ili kupunguza hasara, ni lazima mfugaji ahakikishe kuwa mayai yanafika sokoni yakiwa bado mapya na salama.

Utunzaji sahihi wa mayai huyafanya yaepukane na madhara yanayoweza kutokana na viumbe wadogo wadogo kama vile bakteria, wanyama walao mayai, upotevu wa unyevu, au joto wakati wa uhifadhi na kusafirisha kwenda sokoni, jambo linaloweza kuyafanya yavunjike.

Mayai kama ilivyo kwa viumbe hai wengine yanahitaji kupumua. Trei za kuhifadhia mayai zinapswa ziwekwe kwenye sehemu yenye hewa inayozunguka kwa wingi hasa hewa ya oksijeni.

Trei zote za kuhifadhia mayai ni lazima ziwekwe katika hali ya usafi, zisiwe na harufu ili kuepuka kufishwa au kusababisha hali yoyote inayoweza kusababisha uharibifu. Mayai ni lazima pia yakingwe dhidi ya joto kali pamoja na unyevu.

Mayai yanahitajika kuwekwa katika trei kwa mpangilio ili yabaki na ubora wake, na zifuatazo ni njia rahisi za namna ya utunzaji.

**Weka sehemu yenye ubaridi**

Mayai yanaweza kuharibika kwa haraka kutokana na joto kali. Labda yahifadhiwe kwenye jotoridi la chini, vinginevyo mfugaji atapoteza idadi kubwa ya mayai kabla hayajafika sokoni.

Ni lazima kuhakikisha kuwa mayai yanahifadhiwa sehemu yenye ubaridi, ambayo siyo kavu sana, vinginevyo yatapoteza unyevu kwa haraka endapo yatawekwa sehemu kavu. Hali ya mahali pa kuhifadhia inategemea na siku ambazo mfugaji anahitaji kuhifadhi mayai.

Wafugaji wenye uzoefu wamekuwa na uwezo wa kuhifadhi mayai kwa kipindi cha miezi 6-7 kwa kutumia majokofu maalumu. Wafugaji wadogo pia wanaweza kuhifadhi mayai kwa siku kadhaa mpaka watakapopata mayai kwa ajili ya kuhatamiwa. Kamwe usihifadhi mayai unayokusudia kutumia kwa ajili ya kuhatamiwa kwenye jokofu.

**Uhifadhi wa mayai kwa ajili ya kuhatamia**

Wafugaji wadogo wengi hutumia njia ya kiasili kuhatamishia na kuangua mayai. Hii ni njia ya kutumia kuku au ndege mwingine ambaye hupewa mayai na kuyahatamia hadi kuanguliwa.

Kuku wa kienyeji ni wazuri sana wanapotumiwa kwa ajili ya uzalishaji wa vifaranga. Hata hivyo, kwa uzalishaji mzuri ni lazima mfugaji ahakikishe kuwa kuku anapewa mayai yenye uwezekano mkubwa wa kuanguliwa.

Mbinu moja wapo ambayo mfugaji anaweza kuitumia kutambua mayai yenye uwezekano mkubwa wa kuanguliwa ni kwa kumulika kwa kutumia tochi maalumu. Ingawa kuna tochi maalumu za kumulikia mayai lakini tochi za kwenye simu zinafaa pia.

**Tengeneza sehemu ya kuhatamia mayai**

Mfugaji anaweza kuboresha uzalishaji wa kuku wa kienyeji kwa kuwajengea tabia ya kuhatamia mayai. Kuku wa kienyeji wakiwa wamelishwa vizuri, wanaweza kuhatamia kati ya mayai 10-14 kwenye mzunguko mmoja.

Baada ya kuangua, mfugaji amruhusu kuku kukaa na vifaranga walau kwa wiki moja. Baada ya hapo vifaranga wanaweza kutengwa.

Kuku wakiwa bado katika hali ya kuhatamia, anaweza kupewa mayai ya bandia ambayo yanaweza kutengenezwa kutokana na sabuni, huku kuku wengine wakiwa wamehatamia mayai halisi ya kutosha. Mayai bandia yanaweza kuondolewa na kuku kuwekewa mayai halisi aendelee kuhatamia mpaka yatakapoanguliwa.

Kuku wanaohatamia ni lazima wapatiwe chakula na maji ya kutosha. Kuku ambao hawahitajiki kwa ajili ya kuendelea kutotoa, wanyang'anywe vifaranga na kuachiliwa walipo kuku wengine.

Ni vizuri kuweka alama kila yai kuonesha ni tarehe gani lilitagwa, hii itamsaidia mfugaji kutokuchanganya mayai ya zamani na mayai mapya. Badala yake, mfugaji anaweza kuwatenga kuku ambao amewaandaa kwa ajili ya kutotoa na wale ambao ni kwa ajili ya kutaga tu ili asichanganye mayai yake.

***Imeandaliwa na Godfrey Sanga kwa msaada wa taarifa mbalimbali kupitia mitandao wa kompyuta***



# Maajabu ya tembo pindi wanapokufa watoto wao



**>>>Inatoka Uk. 8**

heshima kwa viumbe vilivyokufa.

Tafiti za awali zilifichua kwamba tembo wa Asia huomboleza kama familia, mtafiti wa Taasisi ya Sayansi ya India Raman Sukumar, aliambia Jarida la National Geographic.

Vivyo hivyo, waliona kwamba wanyama hao waliitikia huzuni kwa kuwabembeleza na matendo mengine ya upendo.



**MBALI NA WANADAMU**

Tayari ilikuwa imeonekana kwamba tembo wa Kiafrika hufanya ibada ya mazishi, wakiwafunika watoto wao kwa matawi na majani, lakini utafiti huu na tembo wa Asia, ni rekodi ya kwanza ya tembo kuweka miili katika nafasi maalum na kuizika kwa udongo, ripoti Live Science.

Tembo wa Asia hawaziki watoto wao popote pale.

Pachyderm huchagua mahali pa pekee, mbali na wanadamu na wanyama wanaokula nyama, huku wakitafuta mifereji ya maji na mifereji ya kuzika maiti," ripoti hiyo inasema.

Miili hiyo mitano iliyofanyiwa utafiti ilipatikana katika maeneo yanayolima chai, mbali na maeneo yenye watu wengi.

Wanasayansi waliifukua miili hiyo ili kuifanyia uchunguzi na kugundua kuwa ilikuwa na umri wa kati ya miezi mitatu na mwaka na baadhi yao walikuwa na utapiamlo au walikuwa na maambukizi.

Michubuko iliyopatikana kwenye migongo ya kila mtoto wa tembo inaonesha kwamba waliburutwa kwa umbali mrefu hadi kwenye maeneo ya kuzikia.

"Kuna ripoti ambazo hazijachapishwa kutoka Idara ya Misitu ya Bengal Magharibi ya tembo jike kubeba mzoga kwa hadi siku mbili kabla ya kuutelekeza katika eneo lililojitenga huko Bengal Kusini," ripoti hiyo inaeleza.

"Viumbe hao wenye hisia, hawaachi maiti hadi ianze kluharibika au hadi maafisa wa Idara ya Misitu wachukue jukumu la kuisimamia maiti," iliongeza.

Tofauti na tembo wa Kiafrika, tembo wa Asia hawarudi kwenye eneo la kuzikia, bali huchagua njia nyingine mbadala za kusafiri.

**TAFSIRI YA KWANZA YA MATOKEO**

Kwa mwanabiolojia na mhifadhi Chase La Due, "utafiti huo ni muhimu, kwa sababu unatoa ushahidi wa kushangaza wa matatizo ya kijamii ya tembo," alisema mwanabiolojia Chase La Due, anayefanya kazi katika Zoo, katika mahojiano na gazeti la New Scientist na Oklahoma City Botanical Garden, USA.

"Wengine wamebaini kuwa tembo wanaonekana kuwa na tabia ya kipekee kwa ndugu zao waliokufa, (lakini) utafiti huu ni wa kwanza kuelezea kile kinachoonekana kuwa ni utaratibu na wa makusudi wa kuzikwa watoto wa tembo baada ya kuletwa kwenye eneo la kuzikwa," alisema LaDue.

Zaidi ya hayo, mtaalamu alitoa wito wa tahadhari wakati wa kutafsiri matokeo haya.

"Maisha ya kiakili na kihisia ya tembo, bado kwa kiasi kikubwa ni fumbo," alisema.

Mwanabiolojia huyo anaeleza kuwa aina hizi za tafiti zinaweza kuruhusu uundwaji wa mikakati mipya ya kuhakikisha uhai wa wanyama hawa.

Tembo wa Asia, ambao huishi kwa wastani kati ya miaka 60 na 70 porini, wako kwenye orodha ya viumbe vilivyo hatarini kutoweka iliyotengenezwa na Muungano wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira.

Inakadiriwa kwamba kwa sasa takribani vielelezo 26,000 huishi porini, hasa nchini India na baadhi ya nchi nyingine za Kusini-Mashariki mwa Asia.

BBC.



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462



# Uwekezaji zaidi kwa wanawake utaongeza kasi ya maendeleo

Kila ifikapo Machi 8 kila mwaka, duniani kote huadhimishwa Siku ya Wanawake. Katika siku hiyo, wanawake katika ngazi mbalimbali hujadili mustakabali wa maendeleo ya wanawake ambapo pamoja na mambo mengine, yanayojadiliwa ni pamoja na mafanikio, changamoto na nini kifanyike ili kumwinua mwanamke zaidi katika nyanja zote za maisha; kijamii, kisiasa na kiuchumi ili kufanikisha azma ya kufikia maendeleo ya kweli.

Kwa mwaka 2024, kaulimbiu iliyokuwa inachagiza siku ya wanawake duniani inasema “Wekeza kwa Mwanamke, Kuharakisha Maendeleo ya Taifa na Ustawi wa Jamii.” Kaulimbiu hii inatoa rai juu ya umuhimu wa familia, jamii, taasisi zisizo za kiserikali na serikali kuwekeza kwa wanawake kwani uwekezaji huo kwa wanawake unao mchango wa moja kwa moja wa kuharakisha maendeleo ya taifa na ustawi wa jamii nzima.

Taifa letu la Tanzania limefanikiwa kutambua umuhimu wa mwanamke katika kufanikisha kufikia maendeleo, ndiyo maana katika alama mojawapo inayolitambulisha taifa letu iitwayo “Nembo ya Taifa” ipo picha ya mwanaume na mwanamke.

Hii tafsiri yake ni kuwa ili kufikia maendeleo ya kweli, ni lazima kuunganisha juhudi za pamoja za mwanaume na mwanawake. Hakuna namna ambayo mipango, mikakati na malengo ya familia, jamii na taifa lolote yanaweza kufikiwa kikamilifu kama wasichana na wanawake wataachwa nyuma bila kushirikishwa ipasavyo.

Kutokana na ukweli ulio wazi kabisa kuhusiana na umuhimu wa ushirikishwaji wa wanawake katika kuharakisha juhudi za kufikia maendeleo, ni lazima kila mmoja kuona umuhimu wa kuwekeza kwa wanawake ili nguvu ya pamoja ya wanaume na wanawake iweze kuzaa matunda ya maendeleo endelevu.

Familia ni taasisi ya kwanza ambayo ikifanikiwa kwenye uwekezaji kwa wasichana na wanawake, taifa letu linapiga hatua kubwa za kimaendeleo kwa haraka zaidi. Wazazi (baba na mama) na walezi ambao ni viongozi katika familia wanalo jukumu la kuwapa nafasi watoto wa kike kupata elimu kwani elimu ndiyo uwekezaji na urithi mkubwa kwa watoto.

Waarabu wana msemo usemao ‘al-ummu madrasa’, kwa maana ya kwamba mwanamke ni shule. Hii maana yake ni kuwa mwanamke mwenye elimu ana nafasi kubwa zaidi ya kulea na kuwapa maarifa watoto wake kwani ndiye mwalimu wa kwanza wa kila mtoto.

Hii inakwenda sambamba na msemo wa Waswahili kwamba ‘ukielimisha mwanaume, umeelimisha mtu mmoja lakini ukielimishe mwanamke, umeelimisha jamii kubwa.’

Hivyo basi, wazazi na walezi wakiwa na utashi wa kutoa fursa sawa za elimu kwa watoto wao wakike na wakiume, ukombozi katika familia hizo utakuwa ni mkubwa kwani watoto wote wa kiume na wakike watasaidia familia zao na kuzikomboa hasa kiuchumi na hivyo kuongeza kasi ya kufikia maendeleo.

Pia, wazazi na walezi wanapaswa kuachana na tabia ya kuozesha watoto wao wa kike katika umri mdogo (ndoa za utotoni) ili watoto wao waweze kufikia ndoto. Ndoa za utotoni ni adui wa uwekezaji kwa wasichana kwani ndoa hizo zinafifisha juhudi za watoto wa kike kupata elimu na hivyo wasichana hao kuanza majukumu mapya ya kifamilia kama vile kuzaa watoto, kuwalea na kutunza waume zao.

Jamii kwa sehemu yao wanayo nafasi ya kuchangia uwekezaji kwa wanawake ili kuharakisha juhudi za maendeleo. Jamii inapaswa kuunga mkono mipango ya kuwainua wasichana na wanawake badala ya kuwa sehemu ya kukwamisha mipango ya maendeleo.

Vilevile, jamii inapaswa kukemea viashiria na vitendo vyote vyenye lengo ya kurudisha nyuma ukombozi wa wasichana na wanawake. Jamii yenye mdomo mpana ikiunga mkono juhudi za ukombozi wa wasichana na wanawake, ni nani anaweza kuzuia na kurudisha nyuma ukombozi wa wanawake?

Serikali ya sasa ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imeonesha utashi mkubwa wa kisiasa kuhakikisha ukombozi wa wasichana na wanawake unafikiwa kikamilifu ili kuharakisha juhudi za maendeleo.

Katika elimu, serikali imetoa fursa kwa watoto wa kike wanaopata ujauzito kuendelea na masomo baada ya kujifungua kwani kupata kwao ujauzito kisiwe kikwazo cha kufikia ndoto walizonazo katika maisha yao. Mara nyingi watoto hawa, kutokana na akili yao kuwa bado hazijakomaa vya kutosha wamekuwa wakirubuniwa kirahisi na wanaume wa hovyo na kujikuta wakiwa na mimba zisizotarajiwa na hivyo hatua ya kuwarudisha shule ni ya kupongeza sana.

Uwekezaji kwenye sekta ya elimu uliopelekea ongezeko la taasisi mbalimbali za elimu kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo na vyuo vikuu, kunaongeza fursa kwa wasichana kupata elimu na hivyo kuchochea juhudi za ukombozi kwa wasichana na wanawake.

Kiuchumi, serikali imeongeza kasi ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, mathalani utoaji wa mikopo ili kuwasaidia wanawake kushiriki katika shughuli za kiuchumi, na hatimaye kuharakisha kasi ya maendeleo nchini.

Kisiasa, wasichana na wanawake wamehimizwa kuthubutu na kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ili wawemo pia katika ngazi za maamuzi na hivyo kuharakisha uwasilishaji wa mikakati inayowanufaisha wanawake moja kwa moja.

Wanawake walioaminiwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi, wameonesha uwezo mkubwa wa kiuongozi na hivyo kuthibitisha kuwa wanawake wanaweza uongozi. Ili nchi yetu iendelee kupiga hatua kimaendeleo kwa kasi kubwa, ni lazima uwekezaji kwa wasichana na wanawake uongezeke mara dufu. Hili likiendelea kufanyika kwa kasi kubwa, Tanzania itapiga hatua kubwa zaidi za kimaendeleo katika kipindi kifupi.

Wanawake oyee.

*Mwandishi ni mwalimu wa Mlali Sekondari iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

# Dondoo za matumizi sahihi ya muda



Matumizi sahihi ya muda (time management) ni moja ya mambo muhimu kuyazingatia ili kufikia hatma unayoikusudia. Watu wengi wamekuwa wakiimba dhana hii bila mafanikio na kujikuta wakipoteza muda mwingi kwa vitu visivyo na matunda.

Tunapoongelea matumizi sahihi ya muda ni kuhakikisha muda wako unatumika kwenye vitu ulivyopanga na vinavyokuletea matokeo. Leo Kliniki ya Fikra inaangazia dondoo muhimu zitakazokusaidia kuutumia muda wako vizuri. Tafadhali Fuatana nami: -

**KUWA NA MPANGO WA MAMBO YAKO (PLAN)**

Watu wengi wanaishi na kufanya mambo yanayokuja tu. Ni muhimu kupanga siku zako na kuhakikisha kila muda upo kwenye mpangilio. Ukiweza kupanga ni hatua kubwa kukufanya utumie muda wako vizuri.

Andaa ratiba yako ya siku, wiki au mwezi na hata mwaka ukionesha mambo muhimu kwa wakati husika, utayafanya lini na kwa rasilimali zipi? Hakikisha una orodha ya mambo yako ya kufanya kila siku (To do List). Tumia kalenda mtandao (Kama vile google calendar), weka vitu vya kukumbusha kama (reminders, alarm, nk.) Dalili ya mtu kufanikiwa ni pamoja na kuwa na mpango rasmi wa mambo yake.

**KUWA NA VIPAUMBELE**

Baada ya kuwa na orodha ya mambo ya kufanya, ni muhimu kuweka vipaumbele ili kujua nini kinaanza na kipi kunafuata. Ni muhimu ukiamka tu, uwe unajua ninaanza na nini na kinachofuatia ni nini?

**ANZA MAPEMA**

Hii ni siri itakayokupa hamasa ya kuutumia muda wako vizuri. Ili kulifanikisha hili; lala mapema, lala saa za kutosha zinayoshauriwa kitaalamu, na ndipo utafanikiwa kuamka mapema na kuanza ratiba zako mapema. Pia ili ufanikiwe vizuri kwenye majukumu yako, anza kwa sala (maombi), anza na mazoezi mepesi kisha anza na mambo rahisi ili kukupa hamasa.

**CHANGANUA KILA JUKUMU LAKO**

Ukijipa jukumu la kufanya, lichanganue vizuri. Mfano ukiweka lengo la mwaka ni kujenga nyumba, basi anza kuchanganua lengo hilo kwenye "tasks" ndogondogo kama vile, lini unatakiwa kununua kiwanja, mpaka lini utanunua matofali, unahitaji simenti mifuko mingapi, nondo ngapi, mbao kiasi gani, gharama ya ufundi ipoje, bati, milango, madirisha, umeme, bomba, nk.

Hapa utakuta ndani ya lengo moja kubwa, kuna kazi au malengo madogo mengi. Haya yatakupa kujua sasa uhalisia wa ugumu au wepesi wa jukumu kuu.

**GAWA MAJUKUMU (DELEGATE TASKS)**

Kama upo na watu, ni vizuri sana ukigawa majukumu. Usilazimishe kufanya kila kitu mwenyewe. Hii itakupa faida nyingi kama kukamilisha mambo kwa haraka, kurithisha uwezo, kuwapa nafasi wengine kukua, itakuongezea uzoefu wa usimamizi, nk.

**WEKA MALENGO JANJA (SMART GOALS)**

Malengo yako ili yatimie hakikisha ni malengo mahsusi (specific), yanayopimika (measurable), yanatekelezeka (achievable), ni malengo halisia (realistic) na pia yawe na muda maalumu na ukomo (time bound). Malengo yenye sifa hizi, hayatakupotezea muda kwenye kuyasimamia kutimia.

**USITOKE NJE YA MALENGO (AVOID DESTRUCTION)**

Ukishaweka malengo ni muhimu sana kuwa makini na mwangalifu ili usitoke nje ya malengo. Hii inaitwa "Focus" Usianze kuvutiwa au kutamani malengo ya watu. Mfano mfano kwenye mitandao ya kijamii, maongezi, wageni wengi na marafiki, kupokea majukumu ya kusaidia na kutamani njia za watu

**SEMA HAPANA KWENYE BAADHI YA MAMBO**

Ili ufanikiwe kutumia muda wako sawasawa lazima uwe na uwezo wa kusema hapana kwenye mambo ambayo hayapo kwenye ratiba zako na hususan yale ambayo hayana mchango chanya kwenye malengo yako.

**SHUGHULIKIA MSONGO WA MAWAZO (AVOID STRESS)**

Ili kutumia muda wako vizuri shughulikia mambo yanayoweza kukutia kwenye msongo wa mawazo au kama tayari upo kwenye hilo tatizo basi shughulikia kwa hekima. Msongo wa mawazo una tabia ya kumpotezea muda sana mhusika na kumwacha kwenye njiapanda kwa muda mrefu.

**USIFANYE MENGI KWA WAKATI MMOJA (MULT-TUSKING)**

Pamoja na kuwa utafiti unaonesha kuwa wanawake wanaweza kufanya mambo kadhaa kwa wakati mmoja, lakini ni vizuri sana ukafanya jambo moja kwa wakati mmoja. Hii itakujenga zaidi kuliko kuwa na mambo mengi kwa wakati mmoja.

**PUMZIKA**

Ukitaka kuwa na matumizi mazuri ya muda, pumzika. Pumzika katikati ya kazi ili kurudisha umakini (Time off – 5 minutes room), fanya mapumziko ya mwili na jiburudishe (refreshments).

**FUATILIA UTIMIZAJI WA MALENGO**

Hii itakufanya usisubiri hadi mwisho wa kazi kugundua kuwa kazi zote zimeharibika uanze upya. Fuatilia kwa nyuma kuhakikisha kila kitu kinaenda vyema na maeneo ya kurekebisha, fanya mapema.

**JITATHMINI (EVALUATION)**

Hili ni jambo muhimu sana kwenye kutunza muda wako sababu bila kujifanyia tathmini za mara kwa mara, utajikuta unarudia makosa yaleyale mara kwa mara jambo ambalo ni upotevu mkubwa wa muda.

Wework Consult - Your Partner in Growth



Na Hamisi Kibari
Mtanzani wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 22

**Dada yake Chris anaamua kuwakabidhi polisi waraka alioandika Chris kuonesha kwa nini ameamua kujiua huku mumewe akijaribu kuzuia hilo bila mafanikio. Chris anapolazwa hospitali ndugu zake mkewe wanafika kumjulia hali na kumweleza kitu ambacho hakuwa anakitarajia. Kwamba wamemsamehe kuhusu suala la kumuua mkewe bila kukusudia na wala hawana mpango wa kumshitaki. Joyce naye anafika wodini na kwa mshangao anasema na yeye hana mpango wa kumshitaki Chris kwa kosa la kufanya jaribio la kumuua. Lakini, licha ya kusamehewa na watu ambao wangekuwa mashahidi kusema hawana mpango wa kumshitaki, Chris anapofikishwa mahakamani anakiri kosa la kumuua mkewe bila kukusudia. Nini mwisho wa mkasa huu? Endelea.**

"Kwa nini umekata tamaa? Kwa sababu ulikiri kosa la kumuua mkeo bila kukusudia? Huwezio kujua msimamo wa Jaji anaweza kukusamehe au usinyongwe. Kwa sababu kama nilimsikia vyema mwanasheria wako, kosa la kuua bila kukusudia halisababishi mtu kunyongwa na kwa bahati nzuri Joye hakukukushtaki. Kesi yake ndio ingekuwa mbaya zaidi."

Kabla Chris hajatoa maelezo yake kuhusu alichokisema dada yake, Jaji aliingia mahakamani. Ilikuwa ni siku ya hukumu ambapo Chris aliamua kutoisumbua mahakama kwa kukiri kosa. Ingawa mashitaka yake yalikuwa ya kuua lakini yeye alisema alimuua mkewe bila kukusudia. Hakutaka kabisa kumhusisha daktari aliyemsaidia kuficha uovu akiamini kwamba hakuwa na sababu ya kumharibia kazi. Aliishia kuimbia mahakama kwamba alimtelekeza hospitali na anaamini alizikwa kama mtu ambaye hana ndugu.

Jaji alikaa kwenye kiti chake cha 'enzi' ana watu wote waliojaa kwenye mahakama ya wazi wakatulia.

Kabla Jaji hajaanza kusoma hukumu, kukatokea sintofahamu mahakamani. Tausi, ama mama Kenny, mtu ambaye wengi walijua ni marehemu akaingia pale mahakamani. Ingawa alikuwa amekitanda ushungi na gauni refu linalofika hadi miguun lakini uso wake ulikuwa wazi.

Chris, dada yake, shemejie na wengineo walishangaa kumwona na wote waliona kama wanaona mzimu wa Mama Kenny. Hali iliyomkuta Chris siku alipomwona Joyce aliyeamini amekufa akiwa wodini ndiyo ilimkuta. Alijikuta pale kizimbani alipokuwa amesimama akpiga kelele na kuianama chini akiamini ameona mzimu.

Hali ile pia ilimshitua Jaji, akijiuliza nini kilikuwa kimetokea na kulazimika kuwaangalia watu waliongia mahakamani pale ambao sasa walikuwa wanatafuta mahaka pa kuketi.

Huku akimtazama kwa mshangao, Mwalimu Misango alikumbuka habari alizoambiwa na Maua kuhusu watu kuona mzimu wa Mama Kenny.

"Mzimu wa Mama Kenny umekuwa ukija mtaani kwetu. Jana ilikuwa mara ya pili kama si ya tatu. Anakuja akiwa katika mtu mfano wa Mama Kenny na gari aina ya IST nyeusi. Bila shaka sisi tunaona ni gari lakini pengine hicho ni kitu kingine… Mtaani hatujawahi kumwona Mama Kenny akiwa amejitanda ushungi, amevaa kama Muislamu anayetaka kuingia msikitini kuswali. Yaani alivaa kama mimi nilivyo."

Kama anayeota, Mwalimu Misango alikumbuka maneno ya Maua.

Mama Kenny aliingia pale mahakamani akiwa ameandaamana na Dokta Nimrod Goima, yule aliyeshirikiana na Chris kuficha kilichodaiwa 'kifo' cha Mama Kenny.

Chris ambaye alikuwa ameinama, alinyanyuka ghafla na kujaribu kukimbia lakini akadhibitiwa na askari.

"Msiogope wala kukimbia. Huyu ni Tausi, Mama Kenny na wala hakufa. Nitaeleza kilichotendeka…" akasema Dokta Goima.

Jaji akapiga meza kutuliza mahakama.

"Msiogope wala kukimbie," alisema Dokta Goima akimwangalia Jaji Waduku Wesai ambaye pia alibaki pia akiwa kashikwa bumbuazi.

Baadaye aliomba nafasi ya kuzungumza. Jaji alifikiri kidogo akauliza tena kama yule ndiye mwanamke ambaye mshitakiwa aliyekuwa kizimbani anatuhumiwa kwa kumuua.

Dk. Goma akajibu kwamba ndiye, kisha akaomba wasaa wa kuzungumza. Jaji Wesai hakmruhusu bali alimgeukia mwendesha mashitaka wa serikali kujua kinachoendelea.

"Huyu ni Mama Kenny na wala hakufa Mheshimiwa Jaji," Dk. Goima alijikuta akirudia tena maneno ambayo aliyasema mwanzo sasa akimwelekea mwendesha mashtak ambaye alikuwa akijiandaa kujibu swali la Jaji.

**Kama huyu ndiye Tausi, basi hukumu hii itakuwa haina maana… hebu tuambie ulichotaka kusema kuhusu marehemu ambaye kwetu amefufuka.**



Jaji alipiga tena meza kutuliza watu baada ya maneno ya Dk. Goima kuamsha zogo. Hali ilitulia na bado watu wakawa wanamwangalia Mama Kenny ambaye alikuwa kanenepa na kunawiri sana bila kuamini macho yake. Mwendesha mashitaka alimjulisha kwamba mwanamke yule aliyekuja na dokta na kusababisha hali kama ya vurumai mahakamani, Ndiye Tausi Chitawo ambaye mahakama ilitaka kutoa hukumu kuhusu kuuliwa kwake na mshitakiwa, Chrysostom Magati.

"Kama huyu ndiye Tausi, basi hukumu hii itakuwa haina maana… hebu tuambie ulichotaka kusema kuhusu marehemu ambaye kwetu amefufuka," alisema Jaji Wesai akimwelekea Dokta Goima. Daktari huyo alikohoa kidogo, kisha akaanza kusimulia. Sasa Mahakama ikiwa imetulia tuli.

Alisema kwamba yeye anamfahamu Tausi siku nyingi kwa maana kwamba walisoma pamoja katika shule ya sekondari ya Uchama iliyoko Nzega, ingawa yeye alikuwa kamtangulia Tausi darasa moja, yeye akiwa kidato cha nne, Tausi alikuwa kidato cha tatu.Dokta akasimulia kwamba, aliamua kumthamini na kumjali Tausi hadi kutengeneza kifo chake ili kumkomoa Chris kwa madhambi yake kwa vile Tausi aliwahi kumwokoa kufukuzwa shule akiwa kidato cha nne wakati rafiki yake Tausi alipomsingizia kwamba kampa mimba, ingawa ukweli ulikuja kujulikana baadaye kwamba alipewa mimba na mwalimu wao."Yule binti alikuwa rafiki ya Tausi… Ukweli niliwahi kumtongoza na kumtaka urafiki wa kawaida. Alipopata mimba mwalimu akamshawishi anitaje mimi na akanitaja. Lakini ninashukuru Tausi ambaye ni mkweli siku zote alisimama imara kusema ukweli kwa sababu alikuwa anajua kilichokuwa kinaendelea kati ya mwanafunzi na mwalimu wake na jinsi ambavyo mimi sikuwahi hata siku moja kufanya naye mapenzi. Kwanza tungefanyia wapi pale shuleni? Bila Tausi, mimi ningefukuzwa shule na leo hii nisingekuwa daktari. Labda ningekuwa mkulima ama mchunga ng'ombe kule kwetu Dodoma."Dk Goima alisema siku Chris alipomleta Tausi pale hospitalini akiwa hajitambui, na bahati nzuri yeye ndiye alikuwa daktari wa zamu, alimkumbuka baada ya kupoteana kwa muda mrefu na hasa baada ya Chris kumtajia jina lake."Mbali na kwamba ninamfahamu, roho iliniuma sana baada ya kugundua kwamba kapigwa namna ile na mumewe. Mimi ni mtu ninayechukia sana mnyanyaso ya kijinsia. Yaani kwa sababu wewe ni mwanaume unajiona una misuli unampiga mkeo, binadamu mwenziyo mithili ya kumuua. Roho iliniuma sana," akasema Dk Goima akimtupia jicho Chris kwa hasira.

*Itaendelea*

# Majeshi ya Marekani, Uingereza yaua 11 Yemen

**SANA'A, Yemen**

WATU 11 wameuawa na wengine 14 kujeruhiwa kufuatia mashambulizi ya anga yaliyotekelezwa na muungano wa Jeshi la Marekani na Uingereza yalilenga miji ya bandari na miji midogo magharibi mwa Yemen juzi Jumatatu, Msemaji wa Serikali ya Yemen inayotambuliwa kimataifa, aliliambia Shirika la Habari la Reuters.

Mashambulizi 17 ya anga yaliripotiwa nchini humo, ikiwemo katika Mji Mkuu wa bandari wa Hodeidah na Bandari ya Ras Issa, kulingana na kituo cha televisheni cha Wahouthi, Al Masirah.

Mashambulizi hayo yamefanyika siku chache baada ya vifo vya kwanza vya raia na upotezaji wa meli tangu waasi wa kiHouthi wanaoungwa mkono na



Iran, kuanza kushambulia meli za biashara Novemba, mwaka jana wakidai kushikamana na Wapalestina wanaoshambuliwa na Israel.

Mashambulizi hayo yamefanyika sambamba na siku ya kwanza ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Licha ya mashambulizi ya kulipiza kisasi ya muungano wa Marekani na Uingereza na majeshi mengine ya majini, Wahouthi walizidisha mashambulizi yao dhidi ya meli za biashara katika moja ya njia yenye shughuli nyingi za usafiri wa meli za biashara duniani.

Wahouthi siku ya Jumatano, waliwaua wafanyakazi watatu wa meli ya Ugiriki ya True Confidence iliyokuwa na bendera ya Barbados katika shambulio nje ya Bandari ya Eden. VOA.

# Waziri Mkuu `aachia ngazi'

**PORT-AU-PRINCE, Haiti**

WAZIRI Mkuu wa Haiti, Ariel Henry, amejiuzulu, Mwenyekiti wa kundi la nchi za Caribbean amesema.

Henry ameamua kujiuzulu kufuatia wiki za shinikizo zinazoongezeka na kuongezeka kwa ghasia nchini humo.

Inakuja baada ya viongozi wa kanda kukutana nchini Jamaica siku ya Jumatatu iliyopita kujadili mpito wa kisiasa nchini Haiti.

Kwa sasa, Henry yuko Puerto Rico baada ya kuzuiwa na magenge yenye silaha kurudi nyumbani.

Aliiongoza nchi hiyo tangu kuuawa kwa Rais Julai, mwaka 2021.

Akizungumza kufuatia mkutano huo mjini Kingston, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Caribbean na Rais wa Guyana, Irfaan Ali alisema:


"Tunatambua kujiuzulu kwake baada ya kuanzishwa kwa Baraza la Mpito la Rais na kumtaja Waziri Mkuu wa muda."

Magenge yenye silaha kali yamedhibiti mitaa ya Mji Mkuu wa Haiti wa Port-au-Prince katika siku za hivi karibuni, yakitaka Waziri Mkuu huyo ambaye hajachaguliwa ajiuzulu.

Henry alikuwa nchini Kenya kutia saini mkataba wa kutumwa kwa Kikosi cha Usalama cha Kimataifa kusaidia kukabiliana na ghasia wakati muungano wa magenge uliposhambulia vituo vya polisi na kuvamia magereza mawili makubwa zaidi nchini Haiti.

Ndege iliyokuwa imembeba Henry, ilizuiwa kutua kufuatia msururu wa mashambulizi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Haiti.

BBC.



Waziri Mkuu wa Haiti, Ariel Henry

# Marekani yauwekea vikwazo mtandao wa Kiislamu Somalia



> Kundi la wanamgambo linalohusishwa na al-Qaeda ambalo wakati fulani lilidhibiti sehemu kubwa ya Somalia la al-Shaabab kama mtandao wa kimataifa.

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imeliorodhesha kundi la wanamgambo linalohusishwa na al-Qaeda ambalo wakati fulani lilidhibiti sehemu kubwa ya Somalia la al-Shaabab kama mtandao wa kimataifa wa utakatishaji fedha na Marekani.

Idara ya Hazina ya Marekani ilisema juzi Jumatatu kuwa inachukua hatua hiyo ikiwa ni kuiunga mkono Serikali ya Somalia katika kampeni yake ya kulidhalilisha kundi hilo baya la kigaidi.

Watu na kampuni 16 katika Pembe ya Afrika, Falme za Kiarabu na Cyprus, wanalengwa na vikwazo vipya vya Marekani ambavyo vinawashutumu kwa utakatishaji fedha na kuwanyima haki ya kumiliki mali nchini Marekani au kuwa na shughuli zozote za kibiashara na raia wa Marekani.

BBC.

**MATAMSHI YA PAPA VITA VYA URUSI, UKRAINE:**

## Ukraine yamwita nyumbani Mjumbe wa Vatican

**KYIV, Ukraine**

UKRAINE imemuita Mjumbe wa Vatican baada ya Papa kusema nchi hiyo inapaswa kuwa na ujasiri wa kuinua bendera nyeupe dhidi ya Urusi.

Askofu Nuncio Visvaldas Kulbokas, aliambiwa Kyiv imekatishwa tamaa na matamshi hayo, Wizara ya Mambo ya Nje ilisema.

Wakati huo huo, Rais Volodymyr Zelensky, amesema msimamo wa Ukraine katika uwanja wa vita, ulikuwa utulivu kufuatia vikwazo vya hivi karibuni.

Hiyo ilikuwa licha ya misaada kutoka kwa washirika wake kwa kiasi kikubwa kuendelea kupungua.

Papa alisababisha hasira nchini Ukraine wakati nakala ya mahojiano na Shirika la Utangazaji la Uswisi RSI, ambayo yanatarajiwa kutangazwa wiki ijayo.

Kwa mujibu wa nakala iliyonukuliwa na Shirika la abari la Reuters, Papa alisema: "Aliye na nguvu zaidi, ni yule anayeangalia hali, kuwafikiria watu na kuwa na ujasiri wa bendera nyeupe na kufanya mazungumzo."

Bendera nyeupe ni jadi ishara ya kujisalimisha kwenye uwanja wa vita.

Hata hivyo, Msemaji wa Vatikani baadaye alisema Papa alikuwa anazungumza juu ya kusitisha mapigano kwa njia ya mazungumzo na siyo kujisalimisha.

Lakini, Ukraine imejaribu kutangaza kutofurahishwa kwake.

Katika taarifa yake kuhusu kuitwa kwa Askofu Mkuu Kulbokas, Wizara ya Mambo ya Nje ilibainisha kuwa badala ya rufaa zinazohalalisha haki ya wenye nguvu na kuwahimiza Urusi kupuuza zaidi kanuni za sheria za kimataifa, Mkuu wa Kiti Kitakatifu angetarajiwa kutuma ishara kwa jumuiya ya ulimwengu kuhusu hitaji la kuunganisha nguvu mara moja ili kuhakikisha ushindi wa wema dhidi ya uovu pamoja na kukata rufaa kwa mshambuliaji na wala si kwa mwathirika."

Ukraine imekuwa na nia ya kuondoa pendekezo lolote kwamba itasalimu amri kwa Urusi zaidi ya miaka miwili baada ya uvamizi huo.

"Hiki ni kipindi cha kuwa makini zaidi, mpango wetu wa kuhakikisha kuwa ni Ukraine ambayo inaamua mwisho wa vita hivi," Rais Zelensky alisema katika hotuba yake ya usiku wa juzi Jumatatu.

"Tunaweza kuvumilia. Lazima tushinde," alisisitiza Rais Zelensky.

Mapema siku hiyo,Rais Zelensky aliliambia Shirika la Utangazaji la Ufaransa la BFM TV kwamba Ukraine imesimamisha kuendelea kwa shughuli za Urusi Mashariki mwa Ukraine. Hata hivyo, madai hayo hayajathibitishwa.

BBC.

# Wajue wanasoka bora ambao hawajawahi kushinda taji la ligi


**Na Valensi Mbaga**

KANDANDA mara nyingi huleta utukufu kwa wachezaji na wote wanaohusika, na wachache sana huwahi kuonyesha viwango vikubwa na kuacha majina yakiishi kwenye vitabu vya kihistoria enzi na enzi.

Walakini, kumekuwa na wachezaji wachache kwa miaka kadhaa ambao wamekaa sawa au hawajawahi kuwa kwenye kiwango cha kutosha kushinda taji la ligi.

Makala hii imepewa msukumo juu ya mgongo wa nahodha wa Uingereza Harry Kane na kuhamia kwake Bayern Munich kwa ajili ya kutafuta taji lake la kwanza la ligi, lakini timu yake imeangukia nyuma ya Bayer Leverkusen katika mbio za ubingwa wa Bundesliga, jambo ambalo linaweka hali hii hatarini.

Wachezaji hawa 10 wana majina makubwa sana katika soka, lakini hawakuwahi kushikilia taji la ligi. Badala yake, wamekumbukwa kama wachezaji bora waliokosa nafasi ya kunyanyua taji la ligi.









**10: DANIELE DE ROSSI**

Kuanzisha orodha, Daniele De Rossi alikuwa mmoja wa wachezaji thabiti na mahiri katika maisha yake yote.

Muitaliano huyo aliimarisha safu ya kiungo ya Roma kila msimu, akifanya kama mchezaji wa mpito kati ya ulinzi na ushambuliaji.

Mchezaji muhimu ambaye mara nyingi hushinda taji, lakini sio De Rossi. Alikuja karibu katika hafla tatu tofauti, lakini Roma hawakupata nafas ya kunyakua taji hilo la ligi.

Katika msimu wa 2016/2017, walimaliza wakiwa na pointi 87 jambo la kushangaza bado wakiwa pointi nne nyuma ya mabingwa wa Italia Juventus. Ilidhihirisha bahati ya De Rossi nchini Italia, kwani, licha ya ubora wake wote, hakuwahi kushinda taji lililotafutwa zaidi nchini humo.

**9: MARCO REUS**

Marco Reus akiichezea Borussia Mönchengladbach alikuwa moja ya kinda machachari zaidi.

Alipohamia Dortmund Reus amekuwa mmoja wa wachezaji wanaopendwa zaidi na wasiopendelea upande wowote tangu alipoanza kung'ara akiwa na Borussia Dortmund mwanzoni mwa miaka ya 2010. Hata hivyo amekuwa akikosa kitu kimoja tu ambacho ni kombe la Bundesliga.

Kwa kawaida, alijiunga na Dortmund mwaka mmoja baada ya kushinda taji hilo na, tangu wakati huo, wamekaribia mara kadhaa. Wamekuwa wakipigiwa upatu kutwaa taji kila mara na Bayern Munich, ikiwa ni pamoja na msimu wa 2022/2023, wakati Dortmund walipotoka sare nyumbani dhidi ya Mainz siku ya mwisho ya msimu na ushindi ungeweza kupata taji, ikiashiria mapambano ya Reus.

**8: FERNANDO TORRES**

Fernando Torres ambae ametumikia timu mbali mbali ikiwemo Atletico Madrid, Liverpool, Chelsea, AC Milan na Sagan Tosunaye ni mmoja kati ya wahanga wa janga hili.

Unapofikiria washambuliaji wazuri wa misimu kadhaa iliyopita, labda unamfikiria Fernando Torres amabae, alikuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani kama ilivyoonyeshwa Atletico Madrid na Liverpool.

Hata hivyo pia alipambana, ikiwa ni pamoja na kipindi kibaya sana akiwa Chelsea. Aliendelea maisha yake yote bila kushinda taji la ligi, licha ya kuja karibu mara nyingi.

Msimu wa 2008/2009, Liverpool walimaliza wakiwa na pointi 86, pointi nne nyuma ya mabingwa Manchester United. Torres alifunga mabao kumi na nne katika ligi msimu huo (14), lakini hata hilo halikuweza kuwasaidia Wekundu hao kuvuka mstari.

**7: GARY LINEKER**

Gary Lineker huwa anatania na Alan Shearer wanapokuwa kwenye TV kuhusu jambo hili wakati wa taaluma zao za kisoka.


Shearer hakuwahi kushinda Kombe la FA, lakini Lineker kwa namna fulani hakuwahi kushinda taji la ligi. Lineker aliihama klabu ya utotoni ya Leicester na kwenda Everton kutafuta mataji, lakini alishindwa.

>>>Inaendelea Uk. 21

# Wajue wanasoka bora ambao hawajawahi kushinda taji la ligi




>>>Inatoka Uk. 20







Msimu wa 1985/1986, walishika nafasi ya pili kwa pointi 86, pointi mbili nyuma ya wapinzani wao Liverpool. Hata alipohamia Barcelona na hatimaye Tottenham - hakuweza kupata taji la ligi, licha ya kuwa mmoja wa wafungaji bora wa wakati wote.

**6: ANTOINE GRIEZMANN**

Antoine Griezmann amekuwa mmoja wa wachezaji wa kufurahisha zaidi kutazama wakati wa kizazi cha kisasa, akiwapita mabeki shida kutokana na ubunifu wake.

Hata hivyo, hajawahi kushinda taji la ligi. Ajabu, Griezmann amejiunga na Atletico Madrid mara mbili kama mabingwa, lakini hajawahi kushinda La Liga akiwa nao. Alikaribiana na Barcelona mara mbili katika kipindi chake kifupi kwenye ufuo wa Mediterania, akiwa na pointi 73 na pointi 82 mara mbili, lakini haikutosha kuwashinda wapinzani wao.

Huku akiendelea kuimarika licha ya kuwa mzee, inabakia kuonekana iwapo Griezmann atawahi kushinda taji la La Liga.

**5: HARRY KANE**

Harry Kane yuko kwenye mwisho wa kupokea utani wa mara kwa mara katika siku za hivi karibuni.

Hajawahi kushinda taji lolote la uchezaji, licha ya kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi ulimwenguni na wa wakati wote.

Kane alikaribia mara mbili ubingwa wa Premier League akiwa na Tottenham. Msimu wa 2015/2016, walizima wakati wa mchujo, na kuwapa ubingwa mabingwa Leicester City.

Mwaka mmoja baadaye, walicheza kandanda bora zaidi kwenye ligi, lakini wakatolewa kwenye reli na Chelsea na mshindi wa mfululizo Antonio Conte.

Ilionyesha kutokuwa na bahati kwa Kane, ambayo ilimfanya ajiunge na Bayern Munich msimu wa joto wa 2023 kujaribu kushinda mataji. Walakini, inaonekana atakosa taji tena katika msimu wa 2023/2024.

**4: GORDON BANKS**

Golkipa Gordon Banks ni moja ya wachezaji maarufu katika mpira wa miguu wakati wote. Banks ni moja ya njia iliyopelekea kumnyima fowadi mashuhuri Pele nafasi ya kuchukua Kombe la Dunia la 1970.

Hata hivyo, licha ya mafanikio yake yote kwa Uingereza kwenye hatua ya kimataifa, hakuwahi kushinda taji la ligi. Tofauti na wengine, Banks hajawahi hata kulisogelea taji hilo kwa karibu.

Timu bora alizochezea ni Leicester na Stoke, huku umaliziaji wake bora wa ligi ukiwa wa nne mwaka wa 1963. Licha ya kutoshinda taji la ligi, bado anachukuliwa kuwa mmoja wa makipa bora wa wakati wote, akizungumzia kipaji chake.

**3: SOCRATES**

Socrates ni mmoja wa wachezaji bora kuwahi kupamba uwanja wa soka. Kipekee, shahada yake ya matibabu na ufahamu wake wa kisiasa, pamoja na mtindo na ubora wa uchezaji wake, vilimpatAia jina la utani "Dokta Socrates," lakini licha ya kipaji chake hakuwahi kushinda taji la ligi.

Serie A ya Brazil ilikuwa na mfumo wa kipekee wakati wa uchezaji wake, mara nyingi ikiishia katika hatua ya mtoano, lakini hakuwahi kukaribia sana taji hilo. Licha ya hayo, uwezo wa Socrates haukuwa na mwisho, kama ulivyoonyeshwa katika nyanja za ndani na kimataifa.

Socrates alitumikia timu kama Botafogo, Fiorentina, Flamengo na Santos.

**2: BOBBY MOORE**

Bobby Moore aliiwakilisha Fulham kabla ya kujiunga na timu za Marekani na Denmark. Aliichezea timu hiyo ya East London kwa zaidi ya muongo mmoja na nusu, lakini hawakuwahi kumaliza nafasi ya sita naye katika safu ya ulinzi.

Moore atakumbukwa daima kwa kuwa nahodha wa England na kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia mwaka wa 1966, lakini licha ya kuchukuliwa kuwa mmoja wa mabeki bora zaidi wa wakati wote kushindwa kwake hata kukaribia umaarufu wa ligi ya nyumbani kumekuwa kikwazo kwenye maisha yake ya soka.

**1: STEVEN GERRARD**

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, Steven Gerrard ni mmoja wa viungo bora wa wakati wote, lakini atakuwa na kivuli kimoja kisichohitajika kinachomfuata milele ambacho ni kushindwa kwake kushinda taji la ligi.

Maafa yake maarufu yalikuja mwishoni mwa msimu wa 2013/2014 wakati Gerrard alipoteleza nyumbani kwa Chelsea na kumzawadia Demba Ba bao na ushindi wa The Blues na kupoteza ubingwa huku Liverpool waliendelea kuporomoka katika mchezo uliofuata na kumaliza nafasi ya pili.

Pia alimaliza msimu wa pili 2008/2009 na msimu wa 2001/2002, lakini walipigwa tena. Alishinda Ligi ya Mabingwa na vikombe vingine vingi, lakini nahodha wa Liverpool kila mara aliteleza katika dakika ya mwisho ya Ligi Kuu.

# Kutoka kwenye muziki wa dansi hadi bongo fleva


Diamond Platnumz

Na Valensi Mbaga

KATIKA kipindi cha miaka ya 1980/1990 kulikuweko na mfumo wa utawala wa shughuli za Utamaduni ambao pamoja na kuweko Maafisa Utamaduni wa Wilaya, Maafisa Utamaduni wa Mkoa, pia kulikuweko na Baraza la Muziki la Taifa (BAMUTA), ambapo kulizaliwa vyama ambavyo vilifanya kazi kubwa katika kuunganisha wanamuziki kama vile CHAMUDATA na Tanzania Taarab Association. Na itakuwa ni makosa kutotaja show iliyokuwa kubwa sana na iliyounganisha wanamuziki wa nchi nzima TOP TEN Show. Show hii iliyowezekana kwa ushirikiano wa BASATA, Umoja wa Vijana, Radio Tanzania, halijawahi kutokea tena onyesho lenye ukubwa wa aina hiyo mpaka leo

Zama hizi ndizo zilizozaa muziki wa kizazi kipya maarufu kama Bongo Flava. Zama hizi kuna mapinduzi makubwa sana katika muziki nchini Tanzania, mabendi mengi ya muziki wa dansi yalianzishwa, hasa kwa wale wakongwe na kuunda bendi zao binafsi. Kukua kwa teknolojia na kuanza matumizi ya kompyuta katika utayarishaji wa muziki.

Hapa hasa vijana ndipo waliposhika hatamu na muziki wa kizazi kipya. Ottu Jazz Band miaka hii walitumia mtindo wa "Discipline" na walitingisha hasa katika miaka hii. Miaka hii ndipo palipoanza kuwa na taasisi au kampuni kubwa-kubwa za uburudishaji wa muziki kama vile Radio One, Clouds FM, Radio Uhuru, Times FM na nyingine nyingi tu.

Sehemu kubwa ya vijana waliozaliwa miaka ya 1980 na 1990 mwanzoni walianza hamasa ya kutaka kuwa wanamuziki na kujishughulisha na kazi muziki kwa kiasi kikubwa sana. Kipindi hiki ndiko kulikotokea makundi mbalimbali ya muziki wa hip hop ikiwa ni pamoja na Gangwe Mobb, Dewplomatz, S.O.S B., Kwanza Unit, Underground Soulz, Hard Blasterz, na wengine wengi tu.

## KIPINDI CHA MIAKA YA 2000/2010

Katika kipindi hiki, muziki uliokuja juu sana ulikuwa "Bongo Flava na muziki wa dansi ambao hasa vijana wapya au wa muda kiasi walirudi kwa kasi katika kipindi hiki. Hapa bendi ambazo zilijaribu katika kipindi cha miaka ya 1990 katikati na mwishoni zilirudi ama zilivuma kupita kiasi. Bendi kama African Revolution iliyokuwa inatumia jina au mtindo wa Chumvi-Chumvi Tutalamba ilirudi na jina la "Tam-Tam" chini ya uongozi wake Kocha wa Dunia Mwinjuma Muumini.


The African Stars Band

Vilevile T.O.T Plus Band, The African Stars, akina Bob Rudala, Jungle Survivors Band na nyimbo yao ya Maprosoo, Malaika Band, Extra Bongo, Double M Sound ya Mwinjuma Muumin, Mchinga Sound, Diamond Sound, Akudo Impact, Inafrica Band na bendi nyinginezo nyingi zilitingisha katika zama hizi. Chuchu Sound Band ni miongoni mwa bendi zilizotamba sana mwanzoni mwa miaka ya 2000. Waliimba mtindo wa chakacha au mduara kwa lugha maarufu. Bendi hii ilikuwa tishio katika mtindo huo. Bila kuisahau Kilimanjaro Connection Band.

Kiufupi, wakati huu ushindani uilkuwa mkubwa sana na wanamuziki au waimbaji wengi walihama kutoka bendi moja kwenda nyingine hasa kwa kufuatia utitiri wa mabendi ya muziki wa dansi nchini. Kipindi hiki ndicho alichokuja mkali wa sauti nchini Tanzania "King of Melody" Christian Bella akitokea nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Kwa upande wa muziki wa kizazi kipya, ukiacha wale walioanza kabla ya 2000, hapa anakuja Dully Sykes, Manzese Crew, Wandava Creek, Wehu Kumi Ngangari (WTEN N), TID, Jay Moe, Ngwair, Daz Nundaz, Madee, Mandojo na Domo Kaya, Mr. Blue, Complex, Dudu Baya, Juma Nature na FSG, A.Y., G.K., Q Chillah, Mwana FA, Lady Jay Dee na Ray C.

Huku Jay Dee na A.Y. ni wasanii wa mwanzo kabisa kuthubutu kutoka nje ya mipaka ya Tanzania katika kufanya muziki na wasanii wa nchi za nje.

## KIPINDI CHA MIAKA YA 2010 - SASA

Katika kipindi hiki, muziki wa kizazi kipya na muziki wa dansi ulibadilka sana. Vijana wengi walikuja katika muziki wa dansi. Lakini Bongo Flava imepiga hatua maradufu.

Msanii kama Diamond Platnumz ameupeleka mbali muziki wa Tanzania nje ya nchi kwa kiasi kikubwa kupita msanii yeyote yule tangu muziki huu ulipoanza. Katika kipindi hiki, rundo la wasaniii wa muziki wa Bongo Flava (walibatizwa kama wabana pua), waliongezeka na kuigana kupita kiasi.

Watayarishaji wa muziki huu waliongeza zaidi. Bongo Flava, ilianza kuchukua miundo mbalimbali ya miziki mingine kama vile Kwaito, Zouk Rhumba, Singeli, Raggae, muziki wa Nigeria hasa waliiga na kadhalika. Na ndicho kipindi kilichoanza na ushamba katika muziki, hasa kwa kuanzisha makundi-makundi kati ya msanii na msanii.

Kwaufupi duniani kote hakuna aina ya muziki kama bongo fleva kwani Mtindo huu unajumuisha aina nyingi za muziki pamoja kama vile hip hop kutoka Marekani, ikiwa na ongezeko la athira ya muziki wa reggae, R&B, afrobeat, dancehal, na mitindo ya asili ya Kitanzania kama vile taarab na dansi, muunganiko ambao umeunda mtindo wa pekee wa muziki pamoja na mashairi kwa kawaida huwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Tunapaswa kujivunia muziki wetu.


Inafrica Band



## Kona ya Urembo

Na Hidaya Machuppa Simu: +255 765 828 219

# Stara na Ramadhani

### Vazi linalofaa kipindi cha Ramadhan



> Katika mwezi huu mtukufu, ni kawaida kwa waislamu kuchagua mavazi ambayo yanafunika miili yao kwa kiasi zaidi, kama vile mavazi yasiyobana na hijabu za wanawake. Hata hivyo, kiasi haihitaji mtindo wa kujinyima

RAMADHANI, ambayo mara nyingi hujulikana na Waislamu kama Ramadan Kareem ni mwezi mtakatifu wa Kiislamu unaojulikana kwa kufunga, sala, na kutafakari. Ni wakati wa kukua kiroho na kujitia nidhamu. Kwa wafuasi wa Uislamu, mitindo na staha vina umuhimu. Makala haya yanachunguza uhusiano kati ya mitindo na adabu kwa mtazamo wa Ramadhani.

Katika mwezi huu mtukufu, ni kawaida kwa waislamu kuchagua mavazi ambayo yanafunika miili yao kwa kiasi zaidi, kama vile mavazi yasiyobana na hijabu za wanawake. Hata hivyo, kiasi haihitaji mtindo wa kujinyima.

Watu wengi hupata njia bunifu za kueleza hisia zao za mtindo huku wakifuata miongozo ya staha. Yote ni juu ya kupata usawa unaokufanya uhisi vizuri, ujasiri, na heshima kwa imani yako. Mitindo na adabu vinaweza kuwepo pamoja, kuwezesha watu binafsi kuonyesha mtindo wao wa kipekee huku wakiheshimu kanuni za Ramadhani.

#### Maendeleo ya mtindo wa Ramadhani

Dhana ya Ramadhani na mitindo sio mpya. Mitindo imekuwa njia ya watu kujieleza na kusherehekea hafla maalum. Kwa miaka mingi, wabunifu na nyumba za mitindo wametambua umuhimu wa Ramadhani na kuunda makusanyo yaliyolengwa kwa mwezi huu mtukufu.

#### Nini usivae wakati wa Ramadhani

Wakati wa Ramadhani, kwa ujumla inashauriwa kuepuka kuvaa mavazi ya kufichua, yanayobana, au yasiyo na kiasi. Hii ni pamoja na mavazi yanayofichua ngozi nyingi, kama vile kaptula, tope za tanki au nguo za juu za chini. Kuchagua mavazi ambayo hutoa ufunikaji wa kutosha na kukuza hisia ya kiasi na heshima ni muhimu. Kumbuka, mkazo wakati wa Ramadhani Kareem ni kutafakari kwa ndani na hali ya kiroho, kwa hivyo kuvaa kwa njia inayoakisi maadili haya kunahimizwa sana.

#### Kwa nini unyenyekevu?

Adabu inathaminiwa sana katika mafundisho ya Kiislamu na ni muhimu kwa Ramadhani. Inajumuisha unyenyekevu wa kimwili na kiasi katika tabia, hotuba, na kuonekana. Wakati wa Ramadhani, watu hujitahidi kuvaa kwa njia inayoonyesha maadili hayo, wakikuza unyenyekevu, heshima, na kukazia fikira urembo wa ndani.

#### Mitindo ya mtindo wa kawaida

Mitindo ya kiasi imepata umaarufu katika miaka ya hivi karibuni, na wakati wa Ramadhani, watu binafsi hukubali mitindo mbalimbali inayopatana na mila zao za kitamaduni na imani za kidini. Hebu tuchunguze baadhi ya mitindo maarufu ya kiasi katika mwezi huu mtukufu:

#### Kufanya biashara ya Ramadhani Kareem

Ramadhani Kareem kweli imezidi kuuzwa katika nchi za Magharibi. Kadiri ufahamu na uelewa wa Ramadhani unavyoongezeka, wafanyabiashara hutambua uwezekano wa soko na kuanza kukidhi mahitaji na mapendeleo ya watumiaji Waislamu katika mwezi huu mtukufu.

Kuanzia kampeni za kipekee za utangazaji zenye mada ya Ramadhani hadi chapa zinazozindua mikusanyiko ya kipekee, uuzaji wa Ramadhani umeenea zaidi. Ingawa wengine wanaweza kuona hili kama maendeleo chanya ambayo inaruhusu chaguzi mbalimbali zaidi na ushirikishwaji, wengine wanaweza kuwa na wasiwasi juu ya uwezekano wa kupungua kwa umuhimu wa kiroho wa Ramadhani.

Ni muhimu kuweka mizani na kukumbuka kiini cha kweli cha Ramadhani katikati ya biashara.

#### Hitimisho

Mtindo na unyenyekevu vinaweza kuishi kwa usawa. Mitindo na adabu wakati wa Ramadhani Kareem huenda pamoja, kuruhusu watu binafsi kueleza mtindo wao huku wakizingatia imani yao. Kwa kuongezeka kwa mkusanyiko wa Ramadhani kutoka kwa wabunifu mashuhuri, sasa kuna chaguo zaidi kuliko hapo awali kupata mavazi ya mtindo lakini ya kawaida.

Jambo la muhimu ni kupata usawa kati ya kubaki mwaminifu kwa imani yetu na kukumbatia mtindo wetu. Kwa hivyo, katika Ramadhani Kareem 2024, wacha tutikisishe mavazi hayo maridadi huku tukidumisha asili ya staha.

### Vazi lisilofaa kipindi cha Ramadhan



> Inashauriwa kuepuka kuvaa mavazi ya kufichua, yanayobana, au yasiyo na kiasi. Hii ni pamoja na mavazi yanayofichua ngozi nyingi, kama vile kaptula, tope za tanki au nguo za juu za chini.


Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Machi 13 - 19, 2024 |

## Wanashindana wenyewe

**Na Mwandishi Wetu**



BAADA ya kuwapoteza Jangwani Mbogomaji kutoka Mbarali, Mbeya wachezaji wa Yanha sasa wanashindana wenyewe kuwania kiatu cha dhahabu.

Katika mechi ya juzi, mabao ya Yanga yalifungwa na Pacome Zouzoua, Mudathir Yahaya, A, Augustine Okrah na Maxi Nzengeli.

Aziz Ki amepanda kwenye usukani wa magoli kwenye Ligi Kuu Bara akifikisha magoli 12 (sawa na Feitoto) huku akitoa 'asisti' sita.

Maxi amefikisha magoli tisa, Mudathir magoli nane huku Pacome akifikisha magoli saba.

## ROBO FAINALI KLABU BINGWA:

# CAF yasikia maombi...






**Na Mwandishi Wetu**

ZILE tambo za aletwe yoyote, sisi ni bora sasa zimefikia mwisho baada ya drool ya robo fainali ya michuano ya Klabu Bingwa Afrika kufanyika.

Yanga wameangukia kwa Mamelod Sundowns ya Afrika Kusini huku Simba wakikutana na Al Ahly ya Misri.

Wawakilishi hao wa Tanzania wanakutana na timu mbili bora kabisa



barani Afrika.

Mamelodi wakiwa mabingwa watetezi michuano ya Klabu ya AFL ambapo walitwaa ubingwa kwa kuifunga Ahly nchini Afrika Kusini.

Ahly wao ndio mabingwa watetezi wa klabu bingwa.

Timu za Tanzania kwa nyakati tofauti walikuwa wakijinasibu kwamba wanahitaji wababe hao katika hatua hiyo.

Wachezaji nane wa Mamelod walikuwa kwenye kikosi cha kwanza cha timu ya Taifa ya Afrika Kusini iliyoshiriki michuano ya Mataifa ya Afrika.

Asec Mimos atacheza na Esperance de Tunis na mshindi atakutana na yule wa Yanga na Mamelod kwenye nusu fainali.

TP Mazembe wameangukia kwa Atletico Du Luanda na mshindi wa jumla atamenyana na Simba au Ahly kwenye nusu fainali.

## Simba yafukuza mwizi kimyakimya



**Na Mwandishi Wetu**

MNYAMA Simba ameendelea na kampeni yake kukwea kileleni baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Singida FG.

Mechi hiyo ilifanyika kwenye uwanja wa Azam Complex, umeifanya Simba kufikisha pointi 42 katika Michezo 18 waliyocheza.

Mabao ya Simba yalipatikana katika kipindi cha kwanza huku mawili yakifungwa ndani ya dakika 10.

Kipindi cha pili Singida walionekana kurudi kwenye mchezo na kuwabana Simba.

Saido Ntibazonkiza alifungua kitabu cha mabao ya Simba katika dakika ya saba na kuandika bao la pili katika dakika ya kumi.

Fred aliandika bao la tatu katika dakika ya 35.

Thomas Ulimwengu aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Deus Kaseke aliipatia Singida bao la kufutia machozi na likiwa la kwanza kwake katika ligi.

## Azam yawapeleka Yanga kwa Mkapa

**Na Mwandishi Wetu**

AZAM FC hawataki 'ujinga' wameamua pambano lao na Yanga Machi 17 lifanyike Uwanja wa Benjamini Mkapa.

Yanga imekuwa ikitumia Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi kama uwanja wao nyumbani. Uwanja huo unamilikiwa na klabu ya Azam.

Maombi ya timu hiyo kutumia Lupaso yamekubaliwa na serikali ambayo awali ilikuwa imezuia kutumika kwa uwanja huo.

Mbali na Yanga, Azam pia watacheza na Simba kwenye uwanja huo huo wa Mkapa.

Yanga imekuwa ikitoa dozi ya tano tano katika uwanja wa Azam inapokutana na timu pinzani.

